YEHOVA-YIRE 2

Asante, Ndugu Roy. Hebu tubaki tumesimama kwa dakika moja wakati tukiomba. Tuinamishe vichwa vyetu, tafadhalini. Na hebu na tuwazie tu sasa kama kuna kitu moyoni mwako ambacho ungependa Mungu akujibu, usiku wa leo, haja fulani, hebu na lijulikane unapouinua mkono wako, na kusema, "Nina haja mbele za Mungu." Sasa hebu na tuviinamishe vichwa vyetu tunapoomba.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunahesabu haya kuwa ni majaliwa makuu, kuja Kwako; tukijua jambo hili, ya kwamba kama tukija katika Jina la Bwana Yesu, tumeahidiwa ya kwamba tungepokea kile tuombacho. Sasa hatuji kwenye Kiti cha Enzi cha Hukumu. Hakika tusingetaka kuja hapo, wala kwenye Kiti cha Enzi cha Haki. Bali sisi . . . tunakuja kwenye Kiti cha Enzi cha Rehema, ambapo tuna—tuna hakika kujibiwa haja zetu. Kwa kuwa, tusingeweza kustahimili hukumu Yako, wala tusingeweza kuishi kwa haki Yako, bali rehema Yako ndiyo tunayoomba. Kwa hiyo tusamehe, Bwana, dhambi zetu. Tunaomba ya kwamba utatujalia hayo, na ya kwamba utakuwa pamoja nasi usiku wa leo, ukijibu kila ombi ambalo mikono hiyo iliwakilisha wakati ilipoinuliwa juu. Unajua kilichokuwa chini ya mkono huo, moyoni. Na, Mungu, hapana shaka ilikuwa ni kwa ajili ya magonjwa, na wokovu, na wapendwa. Tunaomba usiku wa leo, Baba, hasa sana kwa ajili ya hao, ya kwamba utawajalia maombi yao.

3 Sasa tumekuwa tukizungumza juu ya mtumishi Wako mwaminifu, Ibrahimu, tunaendelea naye usiku wa leo, katika safari yake. Tunaomba ya kwamba utatubariki tunaposhuka kwenda kwenye barabara ya mamia ya miaka iliyopita, pamoja na mtumishi mwaminifu ambaye aliliamini Neno Lako. Jalia iwe ni mfano, kama vile Paulo alivyosema katika Waebrania, jinsi Ibrahimu alivyokuwa, mfano. Nasi tunaomba ya kwamba yeye, imani aliyokuwa nayo, itafunuliwa kwetu usiku wa leo; kuliamini Neno la Mungu, wala tusilitilie shaka, Neno moja Lake, bali tuliamini lote, na kuamini kila kitu alichosema. Na jalia tuweze kuzishikilia ahadi hizo alizotupa, na tuwe wana wa Ibrahimu kwa kuwa katika Kristo. Tunaomba haya katika Jina la Yesu. Amina.

Ketini.

4 Ndugu Borders ni mrefu kidogo kuliko mimi, kwa hiyo sina budi kuishusha maikrofoni chini kidogo zaidi. Na ni majaliwa kuwa hapa usiku wa leo katika mkutano huu tena, na kuwaombea wagonjwa, na kufanya lolote Roho Mtakatifu analotuagiza kufanya. Ninataka kusema jambo hili, kwa kusifu.

Katika safari zangu zote kote Marekani, Marekani na Canada, niliona kitu fulani jana usiku kilichonisisimua sana kuliko viti vyote vya magurudumu ambavyo nimeona vikibaki tupu, na mikongonjo yote iliyowekwa chini, vipofu kuona, viziwi kusikia, bubu kunena, wafu wakifufuliwa, daktari alitia sahihi taarifa kuwa "mtu alikuwa amekufa, na akafufuka." Hayo yote yamekuwa ni ya kusisimua sana. Bali nilipowaona watu jana usiku, ambao ni wafuasi wa kanisa, wakiipokea Kweli na kusimama moja kwa moja katikati ya watu, kukiri wamekosea na wako radhi kutenda mema, hilo lilikuwa ni jambo zuri kuliko yote nijuayo.

5 Kanisa, labda Bibi-arusi amechaguliwa tayari. Ni, kumfanya tayari sasa. Kumfanya . . .

6 Uamsho umekwisha. Tunajua hivyo. Hakuna roho ya uamsho tena. Saa mbili za ibada, kila mtu analalamika. Katika uamsho, ni mchana na usiku, wakati wote, hauishi. Uamsho umekwisha. Na kwa hiyo tunaokota tu masazo.

7 Ilimbidi Ibrahimu kutoa jasho kwelikweli mpaka alipopata tabia. Na ndipo wakati alipopata tabia, jambo la pili lilikuwa ni kumtayarisha basi kumlaki bwana arusi. Hilo ndilo jambo la pili. Mnakumbuka ni wakati gani alipompata? Wakati wa jioni, nuru ya jioni.

8 Nikiwakemea wanawake na wanaume, wote wawili, jana usiku; na kuwaona, katika kuliheshimu Neno, wakisimama na kukubali wamekosea, wanataka msamaha wa Mungu, na kuendelea. Hapa ndipo mahali pa kuwa na uamsho. Kama kungekuwako na uamsho wowote niujuao, ungetukia moja kwa moja mahali hapa, mahali ambapo mioyo miaminifu. Kwa nini? Una kitu cha kufanyia kazi, unaona. Kitu fulani . . . Wengi wao wataingiwa na kiburi, hawataki uwaambie habari zake; kumbuka tu, mbegu ya aina hiyo ni mbegu ya kimadhehebu, sio Uzao wa Ibrahimu. Uzao wa Ibrahimu huliona Neno, na huliamini Neno, upesi.

9 Wakati maskini kahaba yule, kisimani usiku ule, yule mwanamke kisimani . . . Kulikuwako na makuhani na waalimu wamesimama pale karibu, wakimwangalia Yesu akitenda, akiwaonyesha ishara Yake ya Kimasihi, ishara ya Kimaandiko, nao wakasema, "Yeye ni Beelzebuli, ibilisi, mpiga ramli."

10 Bali mara Nuru hiyo ilipommulikia maskini mwanamke huyo, wakati Yeye alipomwambia yale aliyokuwa amefanya, alisema, "Bwana, naona kwamba Wewe u Nabii. Nasi tunajua ya kwamba yuaja Masihi, na, atakapokuja, Yeye atatwambia mambo hayo." Unaona, upesi huo Uzao uliochaguliwa tangu awali ukalisikia, kwa kuwa ulikuwa ni Uzao wa Ibrahimu, hakika. Naye akaiona Nuru. Ilikuwa ni Neno. Alijua ya kwamba Neno liliahidi ya kwamba, Masihi ajapo, Yeye angeyafanya mambo hayo, naye akalitambua.

Yesu akasema, "Mimi ninayesema nawe Ndiye."

11 Alikimbia akaingia mjini na kujaribu kuwashawishi wengine. Akasema, "Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo ambayo nimetenda. Je! haimkini huyu kuwa ndiye Masihi mwenyewe?" Unaona?

12 Sasa neno moja tu kwa dada zetu. Daima nimechukuliwa kuwa ni mchukia wanawake, lakini sivyo nilivyo. Unaona? Nilipokuwa mtoto mdogo, nilikuwa na tukio baya sana; bali daima nimekuwa na heshima kuu kwa mwanamke ambaye alikuwa ni mwanamke, mama. Bali sina heshima kwa hao wanaodai kwamba ni wa heshima wala sio. Ninapenda kumwona mama, mama halisi na wa kweli, yeye ni kito cha thamani.

13 Katika siku hii ambapo wanawake wamepotoka, wamepotoka sana katika siku hizi za mwisho. Maandiko yanasema hivyo. Kwa nini? Ni kumalizika kwa wakati. Mnakumbuka upotovu wa kwanza ulikuwa ni nini? Ulikuwa ni mwanamke. Hiyo ni kweli. Na katika siku ya mwisho! Kamwe hatukuwa na jambo hili; tumekuwa na miaka elfu sita ambayo akina mama wamejaribu kudumu akina mama. Sasa wanajaribu kutenda kama mwanamume, wanavaa nguo kama mwanamume, wanakata nywele zao kama mwanamume, na kadhalika. Kamwe hawakufanya hivyo katika wakati mwingine wowote. Biblia inatabiri jambo hili, ya kwamba wangefanya jambo hili katika siku za mwisho. Tumelifikia, upotovu wa wanawake. Si ajabu Biblia ilisema, "Wale walioponyoka kutoka—kutoka—kutoka Sayuni watakuwa na utukufu mbele za Bwana, katika siku hiyo." Unaona, jinsi ambavyo wale watakaoponyoka!

14 Mnasema, "Haileti tofauti yoyote." Inaleta tofauti. Mtu fulani aliniambia si muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham, jambo hilo dogo halileti tofauti yoyote."

15 Nikasema, "Ilileta kwa Paulo. Naye Paulo alisema, 'Kama malaika kutoka Mbinguni akija na akafundisha jambo lingine, na alaaniwe.' Kama wao ni mhudumu, ama malaika, ama askofu, papa, ama chochote alicho, na alaaniwe kama chochote ni kinyume cha Hili." Unaona, hiyo ni kweli kabisa. Wagalatia 1:8, kama ukitaka kulisoma.

16 Naye akasema, "Vema, sidhani . . ." Kasema, "Nimewaona wanawake wakiwa na nywele fupi, walikuwa wapole na wazuri tu sawasawa."

17 Nikasema, "Hiyo ni kweli kabisa, nimeona hilo pia. Bali hilo silo. Unaona, inakubidi kuyafikia yale Biblia iliyosema!"

18 Vipi kama Mungu alimwambia Musa, "Toa viatu vyako," naye akasema, "Bwana, nitatoa tu kofia yangu, badala yake"? Unaona? Inakubidi kufanya kile Mungu anachosema ufanye! Na shida yake ilikuwa, ninayowazia, kile kinachonitia wasiwasi juu ya hilo, ni kwamba wahudumu watavumilia jambo kama hilo! Ni kitu gani? Inaonyesha ni Adamu wa kisasa aliyeenda na mkewe.

Unaona? Mungu anataka Adamu mwingine anayesimama na Neno, na Yeye peke Yake, Neno pekee. Neno ni kweli, kwa vyovyote! Usielekee huko.

19 Kamwe, katika miaka elfu sita, wanawake hawajapata kutamani kuzikata nywele zao, kuvaa kama mwanamume, kupotoka. Tuko katika wakati wa mwisho. Na Marekani, mtu yeyote anayejua unabii, anajua ya kwamba Marekani inawakilishwa na mwanamke. Huu unaitwa "uhuru wa wanawake." Uhuru wa nini? Kufanya apendavyo, dhambi.

20 Mwanamke hawezi kufanya analotaka kufanya. Biblia inasema asifanye. Mwanamke ni zaotuka la mwanamume. Hata hayuko katika ule uumbaji wa asili. Hiyo ni kweli kabisa. Alitolewa kwa mwanamume. Mwanamume alikuwa wote wawili wa kike na wa kiume; Yeye aliondoa hiyo roho ya kike na kuiweka ndani ya ubavu uliotolewa ubavuni mwake. Sikilizeni! Je! mliona wakati Rebeka alipoenda kumlaki Isaka, wakati aliporuka akashuka kutoka juu ya ngamia, yeye aliufunika uso wake? Kwa nini? Yeye alikuwa akija kwenye kichwa chake.

21 Hawajui jambo hilo. Inawabidi kufanya jambo hilo, kwa vyovyote. Je! uliona wakati mwanamke anapoolewa, yeye huufunika uso wake? Kwa nini? Anakuja kwenye kichwa chake. Nalo Kanisa, Kanisa, likiwa ni Bibi-arusi, linapaswa kujifunika kutokana na kanuni yoyote ya imani, linakuja kwenye Kichwa chake, Neno. Kristo ni Neno, Naye ndiye Kichwa.

22 Sasa, marafiki, sitaki kuingilia hayo. Ni—ni—nilikuwa nikiangalia kule leo, kukiwako na vifungu mia tano, zaidi kidogo ya vifungu mia tano, vya mafundisho yenye kilindi juu ya Biblia. Bali ninataka tu kudumu na Ibrahimu kwenye mkutano huu, kwa namna fulani.

23 Mnajua, ninaamini huenda Bwana akaninii, kama ndugu hawajali, na kama kila mtu, ningependa kurudi hapa na kufanya uamsho ambapo mngeweza kukaa kwa muda mfupi, mnaona, ambapo kweli tungeliingilia kindani na kuona barabara. [Kusanyiko linashangilia—Mh.] Asanteni. Asanteni. Asanteni. Ninajua pana samaki hapa, na—na—najua. Nami ninapenda kuvua samaki. Na una nyenzo za kufanya kazi nazo, mtu ambaye ni mwaminifu. Mtu yeyote anaweza kukosea. Hujui; mimi hufa kila siku, kutokana na makosa yangu, na kujaribu kuishi mbele za Kristo. Na mtu yeyote aliye mkubwa vya kutosha, na yuna Roho wa kutosha wa Mungu kutembea na kukubali ya kwamba amekosea, aseme, "Ninataka kilicho cha kweli," nina ujasiri mwingi papo hapo, kwa kuwa, huyo kweli ni Uzao wa Ibrahimu. Wanataka kulijua. Hawalijui wasipolisikia. Bali halina budi kusikiwa kwanza, kasema, "Tutawezaje. . .bila mhubiri? Na mhubiri anawezaje kuhubiri asipotumwa na Mungu?" Hiyo ni Kweli kabisa. Sasa, angalia sasa.

24 Tunarudi kwa Ibrahimu sasa. Afadhali turudi kwake, kwa hiyo, na kuendelea. Mnaweza kunisikia vizuri, huko juu kwenye roshani huko juu? Tunaninii . . . Ni vyema kuona, usiku wa leo, kundi zuri hivi. Ninyi ni watu wazuri sana hapa. Kwa hakika mimi . . .

25 Nilikuwa nikizungumza na rafiki mmoja leo, anayetoka Canada. Bwana alikuwa ameniongoza kushuka kwenda mahali fulani ambapo ilinibidi kuangalia jambo fulani kutukia. Na halafu akisimama . . . Rafiki huyu, nilikutana naye, naye alikuwa akisema jinsi Wamarekani walivyokuwa ni watu wakarimu. Nami nikasema, "Naam, na humu ndani wapo baadhi ya U—uzao uliokusudiwa tangu awali wa Mungu, humu ndani na kandokando ya mahali hapa, na mahali hapa palipo paovu sana." Simaanishi mji wenu hapa. Mji wangu, ninakotoka, ni mwovu tu kama wenu. Lakini ulimwengu wote ni mwovu, lakini makabwela wote wameelea kuelekea Magharibi. Tunajua hilo. Ustaarabu umesafiri nao. Na palipo na ustaarabu, hapo ndipo dhambi inakaa. Hiyo ni kweli. Iangalie huku na huko hapa chini. Hapa ni sehemu ya makaburi ya wahubiri. Hiyo ni kweli. Uangalie Los Angeles, kila kitu na kila dhehebu hushuka kuingia moja kwa moja mle, na kila mtu ana kanuni ya imani, fundisho. Kulipeleka Neno kule, huwezi kufanya hivyo. Umechafuka sana! Hiyo ni kweli. Mashetani, pepo wachafu, moja kwa moja kwenye kiti cha Shetani! Lakini hata hivyo katikati ya yote hayo, kuna Mbegu mle ndani, pia. Na jambo pekee unaloweza kufanya ni kuitawanya Nuru. Na kama yoyote ya Nuru hiyo . . . Kama mna Mbegu humo, itapata Uhai mara Nuru hiyo itakapoifikia. Inakubidi tu kupanda Nuru, ni hivyo tu. Naye Ndiye Nuru ya jioni, tunajua hilo, Neno Lake.

26 Sasa, jana usiku tulimwacha Ibrahimu. Nilianza kwenye—kwenye mlango wa 22, lakini sikuumaliza, kwa maana nilianza kuweka msingi juu ya kile Ibrahimu alichokuwa hapo mwanzo. Nasi tulimwacha jana usiku ambapo Mungu alikuwa akimthibitishia lile agano. Loo, ninapenda jambo hilo. Kupasua kafara, kufanya a—agano na Ibrahimu. Na jinsi tulivyopata . . . Wakati alipomwita Ibrahimu, Naye alikuwa akienda kumthibitishia lile agano, alimwambia achukue wanyama wenye umri wa miaka mitatu, na kuwapasua. Nasi tukapata zile tatu-tatu. Hatuna wakati wa kuziingilia. Jamani, unaweza kudumu kwenye hilo moja, somo hilo moja papo hapo, mpaka asubuhi, hutakuwa umelielezea. Lakini kwa namna fulani unagusia tu sehemu muhimu, na kumtarajia Roho Mtakatifu katika wakati huu kufunua yaliyosalia.

27 Sasa, jinsi ambavyo ukamilifu, ile Dhabihu kamilifu, kamilifu, Mungu alikamilisha katika maisha ya binadamu yale aliyokuwa anaenda kufanya. Tunajua tuna . . . Tulikuwa na Mungu Baba, ambaye alikuwa ni Yehova Mwenye Nguvu. Wakati huo Huyo alikuwa katika Nguzo ya Moto, akawapeleka Israeli

kupitia nyikani. Ndipo Yehova yuyo huyo akafanyika mwili na kukaa miongoni mwetu, katika umbo la Mwanawe aliyezaliwa, akaumba Maskani apate kuishi ndani yake Mwenyewe, Mungu akidhihirishwa katika mwili. Utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani Yake, dhihirisho kamilifu. Ndipo (kupitia katika lile agano) sehemu Yake ya kibinadamu iliondolewa, ikakatiliwa mbali, apate (agano hili) kuutenganisha ule Mwili uliokufa, ile Damu iliyomwagwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na akaufufua na kuuweka kwenye mkono wa kuume, kisha akamrudisha Roho katika Siku ya Pentekoste. Na Uhai ule ule ulioishiwa katika Kristo Yesu hauna budi kuishiwa katika watu wa agano, Uhai ule ule ukifanya jambo lile lile. Yesu alisema katika Yohana 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Sasa, hilo ni kweli ama ni uongo. Halina budi kuwa ni kweli! Kwangu mimi, kila Neno Lake ni Kweli. Kila Neno ni kweli kabisa. Angalia jinsi inavyopendeza Mungu anavyofanya kazi.

28 Na halafu jinsi ambavyo hao wa Baba. . .Kama vile Mathayo alivyosema, "Basi enendeni, mkawafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Unaona? Sasa, Baba. . .Haimaanishi tuna Miungu watatu. Tuna Mungu mmoja katika ofisi tatu (Ubaba, Uwana, Roho Mtakatifu), Mungu yeye yule jana, leo, na hata milele. Hiyo ni kweli kabisa.

29 Sasa angalia jinsi hilo lilivyodhihirishwa vizuri sana kwa Ibrahimu, na jinsi ambavyo Mungu, katika Nuru hii, alipitia katikati ya vipande hivi, akivitenganisha. Kama tu vile ninii. . .Tulichukua jana usiku, jinsi ambavyo wao walifanya mkataba, wakauandika kisha wakaupasua, kwamba havina budi kuumana. Mkataba hauna budi kuumana.

30 Sasa mnaona, enyi marafiki, hilo ndilo ninalojaribu kusema. Hata miongoni mwa watu wetu Wapentekoste, kunatokea huyu ibilisi wa elimu, akijaribu kuwafanya watu. . .Sasa, ninaamini katika karama zote za Mungu. Ninaamini katika kupaza sauti. Ninaamini katika kunena kwa lugha. Ninaamini katika mambo yote ambayo Mungu alisema. Lakini hata hivyo huwezi kutegemea lolote la mambo hayo kwamba ndiyo sababu una Roho Mtakatifu. Unaona, maisha yako hayana budi kuambatana nayo. Unaona? Ninii Yako. . . "Kwa matunda yako unajulikana." Unaona? Na hayo ndiyo mambo yanayonitia wasiwasi siku hizi, kwa sababu ninaliona kanisa langu mwenyewe, kanisa la Kipentekoste, likiwa ule "mfano wa utauwa," likiiacha Kweli. Na ukiwaletea ile Kweli ya Neno, wanaikimbia. Ndipo unawaomba, "Njoni, mketi pamoja nami," hawatakubali. Unaona, inaonyesha kuna kasoro fulani. Hilo ndilo linalonitia wasiwasi. Na, sasa, sio kwamba ninalipinga kanisa langu. Ninaninii. . .

31 Kama nikimpenda Kristo, ingekuwa ni bora zaidi kwangu kujivunia Kanisa Lake kuliko jinsi ningalijivunia Yeye. Kwa maana ni afadhali mngejivunia watoto wangu kuliko kunijivunia mimi. Na, kumbukeni, mara nyingi nimewazia, kama ningalikuwa na matone mawili ya Damu Yenyewe hasa ya Yesu katika sinia, jinsi ningeishika Hiyo, nisije nikaimwaga. Ningetembea kwa uangalifu sana. Bali usiku wa leo nina kuu kuliko hiyo, machoni Pake, nina kitu kilichonunuliwa kwa Damu Yake. Unaona, Yeye aliimwaga Damu Yake kwa ajili yako. Nami nipo hapa kama mhudumu usiku wa leo, nimeshika, ama kuwaelekeza kwenye kikomo chenu cha Milele. Kwa hiyo sitarejea kwenye kanuni yoyote ya imani wala fundisho la sharti; haina budi kuwa ni Neno, maana hicho ndicho kitu kitakachodumu. Imani Yangu imejengwa juu ya Neno, Na Kristo ndiye Neno. Na kama Kristo akifanyika Neno, basi Neno limedhihirishwa yakini miongoni mwetu. Unaona, halina budi kuwa!

32 Sasa, kwa hiyo, ninaamini ya kwamba Mungu wa Agano la Kale, yote aliyokuwa Yeye, aliyamimina ndani ya Yesu Mwanawe. Na yote ambayo Yesu wa Agano Jipya aliyokuwa, Yeye aliyamimina katika Kanisa alilolinunua kwa Damu Yake Mwenyewe. Unaona? "Bado kitambo kidogo na ulimwengu," *kosmosi* pale, utaratibu wa ulimwengu, "hautaniona tena. Hata hivyo ninyi mtaniona," *ninyi*, Kanisa, "kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Ndipo ule Uzima, ule Mkataba, yule Roho aliyetolewa toka kwa Kristo pale Kalvari, anarudishwa na kumwagwa juu ya watu, Uzao wa Ibrahimu, ambao Mungu aliwaahidia. Kumbukeni, haikuwa ni kwa wazao wake wote, bali ni yule "Uzao."

33 Sasa, kuna fundisho la kuchaguliwa tangu zamani ambalo limeoza, ni upuuzi. Lakini kweli kuna kuchaguliwa tangu zamani kwa kweli. Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, aliweza kuchagua tangu zamani kwa kuwa Yeye ana uwezo wa kujua kabla. Mungu hataki kwamba mtu yeyote apotee, bali, akiwa ni Mungu asiye na kikomo, alijua kwamba ni nani ambaye angeangamia na ni nani asingeangamia.

34 Hiyo ndiyo sababu alisema kabla Isaka ama—ama . . . kabla Yakobo ama Esau hawajazaliwa, Yeye alimchukia Esau na kumpenda Yakobo. Kujua kwake tangu zamani kulimfanya ajue ya kwamba Esau alikuwa ni laghai, naye alimjulisha ya kwamba Yakobo aliiheshimu hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza; haidhuru aliipata kwa njia gani, aliitaka. Sasa, wavulana wote wawili, mapacha, waliozaliwa kutoka kwa mama na baba wale wale watakatifu, lakini mmoja alikuwa ni mhuni na huyo mwingine alikuwa ni mwa—mwaminio. Sasa Mungu, kwa kujua Kwake tangu zamani, alijua hilo.

35 Sasa, Mungu, kwa kutangulia kujua, Yeye—Yeye haipangi shughuli Yake kama . . . Usingefanya shughuli yako hivyo, ovyo-

ovyo namna hiyo. Mungu alijua, kwa kutangulia kujua, ni nani angeokolewa, kwa hiyo Yeye akamtuma Yesu kuwashika wale ambao Yeye alitangulia kuona wangeokolewa. Someni Waefeso, mlango wa 1, nanyi mtaona jambo hilo. Unaona? Sasa, hapo.

36 Ndipo anaipeleka Injili Yake na kuipanda, anamtuma Roho Wake kuihuisha. Sasa, wote wawili watakua kwenye shamba moja, Waebrania 6 inatwambia hilo, "Kwamba mvua huja mara kwa mara," Yesu alisema, "juu ya nchi," na mnaona mle ndani, "kuitayarisha, kuilima nchi; bali miiba na michongoma, ambayo hukataliwa, ambayo mwisho wake ni kuchomwa moto." Mnalipata? Sasa kumbukeni.

37 Tutachukua shamba la ngano. Ninyi watu hukuza ngano hapa. Na huu hapa u—ukame unakuja. Hivi hapa vitambaaji ama magugu mliyo nayo hapa, magugu yanayojulikana yakikua shambani; vitambaaji shambani, nyasi maziwa kwenye magurudumu. . .shambani, michongoma shambani. Na ngano imo shambani. Zote mbili zinaona kiu. Na mvua huja si kwa ajili ya magugu, bali kwa ajili ya ngano, bali maskini gugu hilo litasimama moja kwa moja na kufurahi tu kama vile ngano itakavyofurahi.

38 Lakini kwa matunda yao unajulikana. Roho yeye yule anashuka juu ya mnafiki na atapaza sauti na kupiga makelele kama hao wengine, bali maisha yake ndiyo yanayothibitisha kwamba yeye ni nani. Unaona? Nasi tunategemea sana mhemuko. Na leo hii shamba limejaa kila namna ya mihemuko, kila aina ya mihemko isiyo ya kimaandiko na chochote kile. Hakika. Lakini inatubidi kurudi kwenye Neno, Kweli ya Neno. Neno, jinsi lilivyosema!

39 Sasa, Mungu akimwambia Ibrahimu ya kwamba kupitia yeye, lile agano la tatu, na agano la pekee. Yesu alikuwa tu ni thibitisho la lile agano alilofanya na Ibrahimu, Uzao wa kifalme, Uzao wa Roho.

40 Na kwenu ninyi marafiki zangu wa thamani Wakatoliki, mnaposema, "Salamu, Maria, mama wa Mungu," hivi hamwoni aibu? Mariamu angewezaje kuwa mama wa Mungu? Asingeweza kuwa. Mnasema, vema . . .

41 Nilikuwa nikizungumza na mtu fulani hivi majuzi, wanatofautiana. Walisema ya kwamba—ya kwamba Yesu alikuwa ni u—uzao wa—wa Mariamu. Kama Yeye alikuwa ni uzao wa Mariamu; kabla hiyo mbegu haijashuka kupitia kwenye tyubu, ilibidi pawe na mhemuko wa kuishusha. Basi unamfanya Yehova . . . Mnaona vile mnavyomfanya afanye?

42 Mungu, Muumba, aliumba vyote viwili yai na seli ya Damu pia, ndipo akaileta ile Maskani. Wala mwanadamu hakuwa na uhusiano wowote nayo! Ilikuwa ni Mungu peke yake! Hiyo ni kweli.

43 Yeye alikuwa ni mwanamke mwadilifu, hakika. Wapo wengi waadilifu walioketi hapa usiku wa leo. Na Mungu anapomaliza kukitumia kitu chochote, kinaondolewa jukwaani. Wala yeye si mpatanishi. Yeye si mama wa Mungu. Yeye ni mwanamke mzuri, mtakatifu aliyeko Utukufuni, kwa maana alilitumikia kusudi la Mungu. Na kila mwanamke humu ndani ana nafasi ile ile, pengine si kwa njia ile ile, bali kumtumikia Mungu. Unaona? Mungu atakutumia.

44 Yeye alimtumia tu kama kiangulio, bali Mtoto huyo alikuwa ni wa Mungu. Naam, Yeye alikuwa Muumba wa vyote viwili yai na himoglobini pia. Na hiyo himoglobini, hakika, hutokana na jinsia ya mwanamume; Naye alikuwa Muumba wa hiyo. Na Mariamu aliletewa mtoto huyu mchanga bila ya mhemuko wowote, si zaidi ya vile Roho Mtakatifu alivyomfunika na kuumba ndani ya tumbo lake hii seli ya Damu na yai zilizomzaa Mwanadamu, Kristo Yesu.

45 Na hilo lilikuwa ndilo agano ambalo Mungu alikuwa akiandika nalo, Mungu alipofanyika mwanadamu miongoni mwetu, kisha akapasuliwa vipande viwili. Unaona, hao watatu, wenye umri wa miaka mitatu, kisha akapasuliwa. Ndipo Mungu akaenda Nyumbani na sehemu yake moja, kisha akatuma sehemu hiyo nyingine huku chini. Sasa wakati Mwili huo utakapokutana tena, itabidi iwe ni Uhai ule ule ulioutawala Mwili huo uwe ndio Uhai ule ule unaoutawala Mwili huu. Naye alikuwa ni Neno. Naye ni Neno! Unaona? Na kazi ambazo Neno lilifanya wakati huo linafanya jambo lile lile leo. Yeye ni Neno, Neno la Milele. Nalo Neno la Mungu ni la Milele. Vema.

46 Sasa Yeye alikuwa akifanya nini? Akifanya njia, akionyesha, akijua ya kwamba Israeli, ule uzao wa kawaida, ungemkataa; bali akijua ya kwamba ule Uzao wa kifalme, sio kutoka kwenye kujuana kimwili na Sara, bali kutoka kwenye imani aliyokuwa nayo Ibrahimu, ambayo ilimleta Kristo, huo ndio Uzao wa kifalme wa mataifa yote, waliochanganyikana, Bibi-arusi akitoka katika mataifa yote. Ibrahimu, baba wa mataifa, si kwa sababu alikuwa na ninii . . . aliishi na mke wake, Sara, na kumzaa mwana, bali kwa sababu aliliamini Neno. Amina. Jambo ndilo hilo.

47 Sasa tunaona, baada ya jambo hili, tukio hili kuu. Sasa tunaufikia mlango wa 17. Tutajaribu kuufikia wa 22, ikiwezekana. Mlango wa 17. Je! mnaifurahia safari hii pamoja na Ibrahimu? Ninapenda tu kuiangalia. Kwa sababu nini? Kila alichofanya kilikuwa ni mfano mkamilifu wa Kanisa. Mnaamini jambo hilo? Angalieni, Maandiko yote yanatoa mfano wake.

48 Mwangalie Yoeli, kasema, “Itakuwa katika siku za mwisho, ya kwamba Mungu ataimimina Roho Yake.” Jinsi ambavyo madumadu angetokea na kulila kanisa Lake! “Yaliyosazwa na tunutu, parare; na parare, madumadu.” Na ni mdudu yule yule,

mdudu yule yule katika hatua nne mbalimbali. Kila mmoja anakula sehemu moja. Huyu hapa anakuja maskini madumadu ama parare naye anakula ganda, na huyo mwingine anakula tunda, ndi—ndipo wengine wakaja waliounyonya wakaumaliza uhai kutoka kwake. Huo ni wakati . . .

49 Kristo, ule Mti uliokuwa katika Bustani ya Edeni! Kulikuwako na miti miwili katika Bustani ya Edeni. Miti hii miwili iliwekwa mle kwa ajili ya kuzaa. Na wakati . . . Hawa, yeye alikuwa ndiye ule mti wa mauti kama akiguswa. Naye Kristo alikuwa Ndiye ule Mti wa Uzima. Sasa kupitia kwa mwanamke yanakuja mauti; kwa Mwanamume unakuja Uzima.

50 Sasa wakati aliposimama hapa akiongea na wale Wayahudi, alisema, "Mimi . . . nanii wenu . . . "

51 Wao walisema, "Baba zetu walikula mana nyikani kwa muda wa miaka arobaini."

52 Yeye akasema, "Nao, kila mmoja, amekufa! Bali Mimi Ndimi Chakula cha Uzima, Mti wa Uzima, unaotoka Mbinguni kwa Mungu, ambapo mtu anapokila Chakula hiki hatakufa kamwe."

53 Mungu aliwaweka Maserafi pale, wakiulinda ule Mti, asije mtu akaugusa. Sasa amewaondoa Maserafi, wakijaribu kuwasukuma waingie kwenye Mti huo. Siku hizo, wao waliona ono, walitaka kuuendea ule Mti, wapate kurudi bila ya upatanisho. Lakini sasa baada ya upatanisho kufanywa, ibilisi anawapofusha, anawageuza hivi mbali na Mti huo. Angalia.

54 Wakati Kristo alipokuja duniani, Yeye alikuwa Ndiye Mti mkamilifu wa Mungu. Daudi alimwona katika Zaburi ya 1, kasema, "Mti uliopandwa kando ya maji, vijito vya maji." Mito mingi, Maji aina moja; karama nyingi, Roho yule yule. "Majani Yake hayatanyauka."

55 Bali wakati alipokuja duniani, nini kilichotukia? Utawala wa Kirumi uliukata mti huo na kumtundika juu ya mti uliotengenezwa na mwanadamu. Ndipo Mungu akaufufua Mti huo na kuuweka kwenye mkono wa kuume, kisha akamtuma Roho kumfanyia Bibi-arusi, kama vile Adamu alivyopaswa kuwa naye katika Bustani ya Edeni. Na wakati mti huo ulipoanza, ulikuwa ni mti wa Kipentekoste.

56 Tunamsikia papa akisema, "Makanisa yote, yarudi kwenye kanisa mama, pale mwanzo. Rudini Roma!"

57 Namtaka mwanahistoria mmoja, mhudumu mmoja, ama mtu fulani asimame, aniangalie usoni na kunionyesha kwamba kanisa lilianzia Rumi. Kanisa lilianzia Yerusalemu kwenye Siku ya Pentekoste! Hapo ndipo. Madhehebu yalianzia Rumi, miaka mia tatu na kitu baadaye. Bali Kanisa lilianza Pentekoste; Mungu akiuinua mti wa Bibi-arusi kwa ajili ya Kristo, akiwa na Roho yule yule aliyekuwa ndani ya Kristo, akiuinua mti wa Bibi-arusi. Na ni jambo gani lililotukia? Wakati lilipoanza

kuugua, kukua, yule mdudu wa Kirumi aliuparamia na kuanza kuuvunjilia mbali. Yaliyosazwa na tunutu, yameliwa na madumadu, mpaka ukafikia kwenye shina.

58 Lakini Mungu alisema, "Nitarudisha, asema Bwana." Mti huo utachipuka tena, kwa kuwa Mti wa Bibi-arusi unakua kuwa Bibi-arusi.

Ndipo Luther akatokea, yeye alifanya nini? Kufuatilia kuhesabiwa haki.

59 Hivyo ndivyo hasa Kanisa lilivyoingia, Yohana akihubiri kuhesabiwa haki. Ndipo Yesu akaingia, akihubiri utakaso. Waebrania . . . Ninamaanisha Yohana Mtakatifu 17:17, "Watakase kwa ile Kweli, Baba. Neno Lako ni Kweli." Naye alikuwa ni Neno. Hiyo ni kweli. Alikuwa ni ile Dhabihu. Ndipo, kwenye Siku ya Pentekoste, pamoja na Roho Mtakatifu. Kuhesabiwa Haki; utakaso; ndipo wakati mti huo ulipoupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, ulikuwa ni mti mzima wa Bibi-arusi.

60 Warumi waliula wote. Kama tu ulivyoshuka chini, ndivyo ulivyochipuka! Na ulipoanza kukua kupitia Luther, ni kitu gani? Baada ya kifo cha Luther, wao waliuundia dhehebu. Mume huyo alifanya nini? Aliipogoa maskini mizabibu ya kale iliyokufa.

61 Huyoo akaenda, mbali zaidi, huku moyo wa mti huo unakua. Ni mti uliochaguliwa tangu awali! Mbegu hiyo imo mle ndani, haina budi kuja! Ndipo ikachipuka tena, na Wesley akaanza. Nao wakawa na uamsho mkuu chini ya utakaso. Ni kitu gani kilichotukia? Yeye aliupogoa tena, wakati walipounda dhehebu. Kamwe dhehebu halikupata kuamka. Hakuna moja lililoanguka likapata kurudi tena.

62 Ndipo moja kwa moja wakaja Wapentekoste, pamoja na kurudishwa kwa karama. Ulifanya nini? Ukaunda madhehebu! Mungu alifanya nini? Akaupogoa!

63 Lakini Yeye alisema nini? "Nitarudisha, asema Bwana." Atatoa kutoka kwenye lundo hilo, Kanisa lililooshwa kwa Damu, lililonunuliwa kwa Biblia, na lililo imara kwa Neno, Bibi-arusi! Nuru za jioni zinatokea. Tunda huivia wapi? Moja kwa moja juu ya mti. Mimi hapa naenda tena!

64 Turudi kwa Ibrahimu, nyuma, hebu turudi kwa Ibrahimu. Huyu hapa anakuja, Uzao wa kifalme wa wakati wa jioni ukiingia. Mataifa . . . Angalieni sasa baada ya mlango wa 17, tunaona hapa katika mlango wa 17, Mungu alimtokea Ibrahimu katika Jina la Mwenyezi Mungu.

65 Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka tisini na tisa, na wakati huu wote hakuwa ametikisika, bali aliliamini Neno la Mungu; na kuyaita mambo yasiyokuwapo kana kwamba yalikuwapo, maana Mungu alisema hivyo, angali akiamini ya kwamba mtoto huyo mchanga angekuja, akiishikilia ile ahadi. Ni mtu wa jinsi

gani! Ni Ndugu wa namna gani! "Ibrahimu, ambaye pasipokuwa na matumaini . . ." Tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa. Mumewe alikuwa hawezi kuzaa. Mwili wake umekufa. Biblia ilisema ulikuwa umekufa, ya kwamba mwili wake ulikuwa kama uliokufa. Na tumbo la Sara lilikuwa limekufa. Na sasa alikuwa karibu sana amepita wakati wa kukoma hedhi kwa miaka arobaini, na Ibrahimu angali aliamini, ya kwamba mkewe angempata mtoto kwa sababu Mungu alisema hivyo. Haya basi. Kulishikilia Neno kwa maana Mungu alisema hivyo! Haidhuru nini, kanuni za imani zilizolifunika, na, bado hilo Neno lilikaa pale! Ililibidi lije. Na hilo Neno likiwa moyoni mwa Ibrahimu!

66 Haidhuru ni wangapi wanaosema, "Siku za *hii* zimepita, na *ile* pale." Mradi tu hilo Neno liko pale, litaumba, kwa sababu ni Neno lililorutubishwa. Kwa kuwa, Mungu ni Neno, na Uzima wa Mungu umo katika Neno. Angalieni sasa wakati hilo Neno linapoingia katika Uzima wa Mungu, jambo fulani linatukia, linakuja kutimia. Sasa angalieni.

67 Ndipo akamtokea katika Jina la Mwenyezi Mungu. Sasa, Mungu ana majina saba ambatani ya ukombozi. Naye alimtokea hapa katika umbo la Mwenyezi Mungu, ambalo linamaanisha "El Shadai." Katika . . . "Shadai," katika Kiebrania. *El* linamaanisha "mwenye nguvu." *Shad* linamaanisha "ziwa," kama ziwa la mwanamke. Na sasa badala ya kuwa "shad," umoja; "Shadai," wingi. Sasa ni faraja tamu ya jinsi gani kwa mzee, mwenye umri wa miaka mia moja, akilishikilia Neno la Mungu moyoni mwake, na hapa Sauti ya Mungu inamjia na ikasema, "Mimi ni El Shadai. Mimi ni Mungu mwenye maziwa."

68 Loo, ni faraja jinsi gani tuliyo nayo! Sasa, sio, kumbukeni, sio tu "ziwa," bali "mwenye maziwa"! "Alijeruhiwa kwa makosa yetu; kwa kupigwa Kwake sisi tumeponywa."

69 Sasa, mama hufanya nini, akiwa na mtoto wake mchanga, wakati akiwa mgonjwa na anahangaika? Yeye humchukua maskini mtoto huyo. Anamshikilia kwenye ziwa lake, naye . . . ananyonya nguvu za mamaye zinaingia mwilini mwake kupitia ziwa hilo. Na sio tu anaridhika ama yeye ananinii . . . Anatulizwa. Analia kwa sauti yake yote, anasumbuka sana; bali wakati mama anapomchukua na kumweka . . . kumweka kwenye ziwa lake, na kuanza kumwimbia, kumtikisa huku na huko, anamhisi mama yake, kichwa chake kimo kifuani mwake, naye anaanza kumnyonya na anapata nguvu kutoka kwa mama yake, zinaingia mwilini mwake. Yeye anajirudishia nguvu zake, akiongezeka nguvu; na pia anashiba, huku siku baada ya siku anapata nguvu zaidi na zaidi.

70 Ni tukio la namna gani kwa Uzao wa Ibrahimu! Yeye angali ni Mwenyezi Mungu, El Shadai! Tunaweza kushika ahadi yoyote aliyoitoa katika Biblia. Uzao Wake, watoto Wake, kama wewe ni mgonjwa, shikilia tu ziwa la ahadi ya Neno lililosema, "Kwa

mapigo Yake sisi tumeponywa." Inaridhisha! Nasi tunanyonya daima, nguvu zetu, kutoka kwa Mwenye nguvu, El, Mwenye nguvu, Wa Milele, tunaunyonya Uzima Wake kutoka Kwake, kupitia ahadi Yake.

71 Ni hisi ya jinsi gani anayoipata mtu wakati akilala kifuani mwa El Shadai, akiamini, tukijua ya kwamba tunazinyonya nguvu za Kristo, kutoka kwenye ahadi Yake, kuingia ndani yetu!

72 Wakati El Shadai alipomwegemeza Ibrahimu kifuani Mwake, miaka ishirini na mitano hapo kabla; mzee, mwenye umri wa miaka sabini na mitano, na mke wake sitini na mitano; kamwe hakuliacha Ziwa hilo. Alitembea moja kwa moja kwenye nchi ya kigeni, miongoni mwa watu wageni wasiomjua Mungu, bali daima alitoa ushuhuda na alikuwa hodari katika imani, akimsifu Mungu, kwa kuwa alijua alikuwa akinyonya kutoka kwenye hiyo ahadi.

73 Ni tumaini la jinsi gani kwa kanisa usiku wa leo, katika saa yenye giza, ushirikina, mhemuko, ya elimu ya hali ya juu. Roho Mtakatifu alisema, "Katika siku za mwisho kanisa la kielimu litatokea. Roho anasema waziwazi," Timotheo wa Kwanza 3, "katika siku za mwisho wengi watajitenga na Imani, wakisikiliza roho zinazoshawishi, na mafundisho ya mashetani," hakika, "wenye mfano wa utauwa." Walikuwa wakifanya nini? "Wakaidi, wenye kujivuna." Daktari Ph.D., LL.D., QST, sifa hizi zote. "Mbona, Daktari *Nanii*, wakati *fulani*, ni machungaji wetu."

74 Afadhali mwanamume fulani awe katika familia yangu, ama mtoto wangu, ambaye hakujua tofauti kati ya maharagwe yaliyopasuliwa na kahawa, na alimjua Kristo! Hiyo ni kweli. Nimchukue huko nje mahali fulani karibu na kisiki cha kale na kupiga magoti na kuomba pamoja naye mpaka Roho Mtakatifu aingie ndani yake. Afadhali nipate hilo kuliko saikolojia yote ungaliweza kummwagia kwa digrii ya udaktari. Mwambie Neno la Mungu! Naam.

75 "Lakini wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu, wasiofanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, na wasiopenda walio wema."

76 Loo, unasema, Hao ni Wakomunisti." La, la! Hao ni wanaojiita Wakristo.

77 "Wenye mfano wa utauwa, bali wakikana Nguvu zake, hao nao ujiepushe nao. Kwa maana katika hao wamo wale wajiingizao katika nyumba za watu, na kuwachukua mateka wanawake wajinga, waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi, wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli." Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo ilivyo. Nasi tunaiona siku hiyo.

78 Na ni faraja ya jinsi gani kwa mwaminio, kujitenga na kutokuamini kote, kanuni zao zote za imani za kikafiri, mafundisho yao yote ya kikafiri, na kuangalia moja kwa

moja kwa Kristo na kulichukua Neno, na kulishikilia hilo Neno mpaka unaliona likidhihirishwa. Haidhuru inakubidi kungojea kwa muda gani, dumu pale! Mungu aliahidi jambo hilo. Alikuongoza kwake, lishikilie! Dumu pale. Usilighairi. Dumu pale pale. Kama una hakika nalo, utadumu pale. Bali kama unayumbayumba, utaachilia kila kitu kidogo. Tumbili hunyakua vitu vinavyometameta, bali dubu hushikilia alichoshika. Kwa hiyo, shikilia! Naam, wewe shikilia, shika vizuri!

79 El Shadai! Yeye alisema, “Mimi ni El Shadai. Ibrahimu, mimi ni Mwenye nguvu. Wewe ni mzee. Una umri wa miaka mia moja sasa, nguvu zako zote zimekwisha; lakini Mimi ni Nguvu zako! Tumaini lako limekwisha kabisa, bali mimi ndiye Tumaini lako!”

80 Loo, unateseka, usiku wa leo, hapa nje kwa kansa na kadhalika, hivi huwezi kuona mahali Nguvu zako zinakotoka? Sio kutoka kwenye kisu cha daktari mpasuaji, bali kutoka kwenye Neno la Mungu! “Mimi ni Fungu lako! Mimi ndiye Nguvu zako! Unatoa nguvu zako kutoka Kwangu!”

81 Sio kumdharau daktari mpasuaji sasa; yeye hutekeleza sehemu yake ambayo inamhusu. Bali Mungu Ndiye Mponyaji. Hakuna daktari mpasuaji, hakuna daktari, hakuna dawa inayoponya kamwe. La, bwana, hawana dawa hata moja itakayoponya. Sasa, daktari yeyote atakwambia jambo hilo. Wana usaidizi, bali Mungu ndiye Mponyaji. Huenda wakakata jeraha kubwa mkononi mwako, bali inabidi Mungu kuliponya. Hawana kitu cha kujenga tishu; kama wangaliweza, wangalimuumba mwanadamu. Kwa hiyo unaona, Mungu ndiye Mponyaji. Unaweza kuuweka mfupa vizuri, bali inabidi Mungu auponye. Mungu ndiye Mponyaji, “Mimi Ndimi Bwana niyaponyaye magonjwa yenu yote.” Wala huwezi kulifanya Neno la Mungu liseme uwongo; litarudi moja kwa moja kwenye ile kweli kila wakati, litarudi tu moja kwa moja. Huwezi kulifanya liseme uongo.

82 Sasa watu wanasema ya kwamba Biblia hujipinga Yenyewe. Nimetoa changamoto, na kuwaambia watu ningewapa mishahara ya mwaka mmoja hudumani, kama ningeweza, chochote ninachoweza kufanya, kunionyesha neno moja katika Biblia linalopinga lingine. Hiyo ni kweli. Halipo. Ni kwa sababu nia yako ya kimwili inaliangalia jinsi inavyoliangalia. Roho Mtakatifu Ndiye Mfasiri wa Neno hilo. Neno hilo ni kweli, linakaa pamoja. Lote liko pale kama mchezo-fumbo, bali linamhitaji Roho Mtakatifu kuliunganisha pamoja, kuifanya picha ya ukombozi wa Mungu na baraka Zake kwa watu Wake. Amina. Halijipingi! Hakuna hata Andiko moja, hata kifungu kimoja Chake, kinachopinga kingine. Kama kikikipinga, hakina thamani ya karatasi kilimoandikwa, ni kidanganyifu. Mungu

hadanganyi. Mungu ni wa kweli, mwenye haki, mtakatifu, mkweli. Yeye ni Mungu.

83 Sasa, wakati Ibrahimu alipolipata hili neno, ya kwamba "Mimi ni El Shadai. Mimi ndiye Nikupaye Nguvu zako! Mkeo, tumbo lake la uzazi tayari limekauka, yeye amepita kukoma hedhi kwa miaka arobaini, mwili wako ni kama uliokufa; bali Mimi ni El Shadai." Yeye alimleta tu Ishmaeli, mwajua; bali Yeye alisema, "Huyo siye. La, yeye atakuwa ni mtu mkuu. Yeye atawazaa watawala wengi sana. Bali yule niliyefanya naye ahadi, ni kati yako na Sara." Jambo ndilo hilo! Amina. Ibrahimu alijisikia vizuri sana.

84 Akasema, "Sasa ninataka kukwambia jambo fulani, Ibrahimu. Nitalibadilisha jina lako." Akasema, "Hutaitwa Abramu tena, bali Ibrahimu." *Abramu* linamaanisha "Baba mkuu—mkuu." Bali *Ibrahimu* linamaanisha "baba wa mataifa." Na sio S-a-r-a-i tena; yeye ni S-a-r-a, *Sara*, "binti mfalme." Akabadilisha jina lao! Ni ji—jina la jinsi gani lililobadilishwa! Jambo fulani lilitukia kwa sababu wao wananinii. . .Mnaona, hapana budi kuwe na badiliko kabla ya mambo kutukia. Asingeweza kuwapa mtoto mradi tu jina lao lilibaki hivyo.

85 Wala huwezi kuzaliwa mara ya pili mradi tu jina lako lingali nje ya Kitabu cha Mbinguni. Unaweza ukaliandika kwenye kila kanisa, Methodisti, Baptisti, Presbiteri, ukilichukua kutoka mahali pamoja hadi pengine, ukizozana na hao wote, bali itabidi liandikwe kwenye Kitabu cha Mbinguni kabla jambo lolote kuweza kutukia, na uumbaji mpya uweze kuja. Kabla uhai mpya kuweza kuja, ilibidi majina yao yabadilishwe. Huenda ikakubidi kubadilisha lako, pia, kutoka kwenye baadhi ya hivi vitabu vilivyoandikwa na binadamu, kuliingiza kwenye Vitabu vya Mbinguni.

86 "Na hapo, jina lako si *Abramu* tena, 'baba mkuu'; bali ni *Ibrahimu*, 'baba wa mataifa mengi.' Sio tena (Sara), *Sarai*, bali Sara, 'binti mfalme.'"

87 Loo, sisi hapa tunakuja sasa kwenye mlango wa 18. Kutoka wa 17, hebu twendeni moja kwa moja kwenye wa 18, maana ni ninii tu. . .Sitaki kwenda mbali sana nao usiku wa leo, kuwawekeni hapa, maana ninawataka mrudi kesho usiku. Sasa angalieni. Nasi tutafikia, upesi tu tuwezavyo, kwenye mlango wa 22. Angalia sasa. Wakati ilipofikia siku moja yapata, labda, tuseme, siku mbili ama tatu baadaye, Ibrahimu na Sara, hema zao zilipigwa.

88 Huko chini kabisa mjini kule chini, ninawazia Bibi Lutu alikuwa anavaa nguo zote za fesheni mpya walizokuwa nazo kule chini. Naye alikuwa akitengeneza mitindo yote ya nywele na kila kitu walichokuwa nacho. Alikuwa akiishi tu kwa anasa, na kuwafanya binti zake wote wafanye vivyo hivyo. Ni vile vile

tu ambavyo maskini mama kahaba wa kale amefanya siku hizi, na kuwafanya binti zake wote kufanya jambo lile lile.

89 Sasa, lakini Sara, akiwa bado ndiye mwanamke mrembo kuliko wote kote nchini, aliketi katika nchi kavu, kwa sababu alikuwa akimshikilia yeye aliyekuwa na ile ahadi. Sasa afadhali niliachie papa hapa, maana nitaenda, nitakuwa . . . nitawaweka hapa mpaka usiku wa manane. Yeye alimshikilia Ibrahimu. Hiyo ni kweli. Alikuwa na ahadi.

90 Mshikilie Kristo, Yeye ndiye aliye na ahadi! Yeye Ndiye ile Ahadi. Yeye ndiye ile Ahadi! Angalia.

91 Siku moja jua lilichomoza likiwa kali sana asubuhi moja, Ibrahimu alikuwa ameketi huko kwenye kivuli cha hema yake pale karibu na mwaloni. Ndipo akaangalia chini, hapana budi ilikuwa ni karibu na saa tano, naye akawaona wanaume watatu wakija, wakitembea, mavumbi nguoni mwao. Ndipo Ibrahimu akatoka nje mbio. Kulikuwa na kitu fulani moyoni mwake kilichomfanya ajisikie vizuri sana, ndipo akatoka nje mbio na kuanguka miguuni mwao. Basi angalia, yeye akasema, "Bwana wangu!" Hilo si ni la kushangaza? Wakiwa watatu; lakini "Bwana wangu"!

92 Mwangalie Lutu. Wakati wawili kati yao waliposhuka kwenda kule, wawili tu kati yao, yeye alisema, "Bwana zangu." Lutu aliwaita "mabwana." Ibrahimu . . . Lutu aliwaita, wawili, "mabwana."

93 Naye Ibrahimu akawaita, hao watatu, "Bwana! Bwana wangu!" Amina! Loo, wakati umewadia! Angalieni, yeye alisema, "Bwana wangu, kama nimepata neema machoni Pako, njoni huku, mkaketi chini ya mwaloni huu. Hebu nikalete maji kidogo, na niwaoshe miguu Yenu, kisha mle kipande kidogo cha mkate. Kwa sababu hii ndiyo sababu tu Mmepitia hapa, kuniona mimi." Wakaenda kule.

94 Alitoka akaenda kupitia nyuma ya hema, na kusema, "Sara, kanda unga upesi, na uoke mkate mekoni." Akatoka akamshika ndama mdogo, na akamchinja na kumwandaa, na akafanya mishikaki, kisha akaleta siagi na maziwa, na—na akamwandalia mtu huyo, nao wakala.

95 Na Mmoja wao alikuwa ni Mungu Mwenyewe! Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Sasa endapo unataka kubishana Nayo, endelea. Yeye alimwita "Elohimu, Mungu." Alipaswa kujua; alikuwa akizungumza na Yeye. Angalia, "Bwana Mungu!" Sasa, Mmoja wao alikuwa ni Mungu. Naye akamwangalia. Ibrahimu akatambua jambo hilo. Sasa angalieni hapo.

96 Mhudumu mmoja aliniambia siku moja, akasema, "Ndugu Branham, usiniambie kwamba unaamini hilo, ya kwamba Mtu huyo alikuwa ni Mungu?"

97 Nikasema, "Ibrahimu alisema ndivyo alivyokuwa. Watafsiri wote wamelitafsiri vile vile, herufi kubwa za B-w-a-n-a. Na mtu yeyote anayeisoma Biblia anajua herufi kubwa za B-w-a-n-a ni Elohimu. Linatokana na neno lile lile, Elohimu! 'Hapo mwanzo, hapo mwanzo, Mungu aliumba,' Elohimu, Mwenyezi, anayeishi kwa nafsi Yake, 'aliziumba Mbingu na nchi.' Huyo hapo tena, amesimama moja kwa moja mbele zake."

Akasema, "Vema, unajua," kasema, "huyo—huyo alikuwa ni mwanadamu tu."

98 Nikasema, "Hakika, Yeye alikula nyama, Yeye alikula, akinywa maziwa, Naye—Naye—Naye akala mkate." Nikasema, "Hakika, Yeye alikuwa ni Mungu."

Akasema, "Lingewezekanaje?"

Nikasema, "Bwana, wewe—wewe. . . "

99 Mimi—Mimi natumaini hawakuudhi; walikuwa ni Mashahidi wa Yehova. Naye akaniambia, akasema, "Vema, Bw. Branham, angalia hapa, ninataka kukwambia jambo fulani. Mungu asingeweza kufanya hivyo."

100 Nikasema, "Wewe humjui tu Mungu wangu. Hivyo tu." Nikasema, "Mwili wa mwanadamu umeumbwa na nini? Petroli, potashi, na nurulimwengu, elementi kumi na sita. Jambo pekee ambalo ilimbidi Mungu kufanya ili ashuke chini akauchunguze Sodoma, Yeye alisema. . .alinyosha tu mkono na kujichukulia konzi ya nurulimwengu na petroli, na 'Whiu!' Kasema, 'Njoo hapa, Gabrieli, ingia humu ndani.' Hiyo ni kweli. Akanyosha mkono akachota konzi nyingine ya mavumbi, 'Njoo hapa, Mikaeli, ingia humu ndani.' Kisha akajifanyia Mwenyewe mmoja." Ilimbidi awakilishe kitu fulani atakachokuwa katika siku za mwisho, kwa hiyo anashuka chini moja kwa moja na kunena katika mwili wa kibinadamu. Kweli kabisa. Loo, nina furaha sana kwamba Yeye ni wa namna hiyo!

101 Siku moja huenda hata kusiwe na kitu chochote changu kilichosalia. Mimi nimeumbwa kwa hizo elementi kumi na sita, pia. Nilikuwa nikichana nywele zangu mbili ama tatu zilizosalia, hivi majuzi. Mke wangu akaniangalia, naye akasema, "Billy, unapata upara."

Nikasema, "Mpenzi, sijapoteza hata mmoja."

Akasema, "Ulikuwa na nywele za kipilipili."

Nikasema, "Naam, bali sijapoteza hata mmoja wa hizo."

Akasema, "Naomba uniambie ziko wapi."

102 Nikasema, "Basi, mpenzi, hebu uniambie zilikotoka kabla sijazipata. Na kokote zilikokuwa kabla sijazipata, ziko huko zikiningojea niziendee."

103 Amina! Utukufu! Biblia ilisema, "Hakuna hata unywele mmoja wa kichwa chako utakaoangamia!" Haleluya! Hiyo ni

kweli kabisa. Haukuwako, hata hivyo upo; na hata hivyo haupo, kisha upo. Kweli. Hakika! Petroli, nurulimwengu, kalisi, potashi, kadhalika. Mungu. . .Wakati si kitu mimi, si kitu unachoweza kukiona, ni majivu tu, Yeye atanena, haleluya, akizitupa hizo potashi na petroli pamoja, nami nitaishi tena katika Uwepo Wake. Haleluya! Yeye hutupa Uzima wa Milele. Amina. "Wote alionipa Baba, hakuna aliyepotea, Nami nitamfufua tena katika siku za mwisho." Ninaamini hilo! Kama Uzao wa Ibrahimu, ninaitazamia siku hiyo! Ninautafuta Mji Ambao Mwenye Kuujenga na Kuubuni ni Mungu. Amina. Hakika. Haidhuru huu unavyoingia makunyanzi na kupindana, na nywele zinanyonyoka, haidhuru ni jambo gani linalotukia, Mungu atauinua tena, katika fahari ya ujana tena, katika siku hiyo ya mwisho. Yeye aliahidi atafanya jambo hilo, nami ninautazamia Mji huo! Amina. Loo, jamani! Ninajisikia wa kiroho sana sasa hivi, nikijua, na tumaini hilo lililobarikiwa likiningojea Kule. Ninautazamia Mji huo. Moyo wangu unadunda ukielekea huko. Loo, sitageuka upande mmoja, bali nitaangalia moja kwa moja mahali Pale. Mungu, nisaidie kukaa barabara pale, mwadilifu na mwaminifu, nikiirusha kambaokozi, kila mahali, na kumleta kila msafiri aliyechoka niwezaye, kuendelea na safari.

104 Naam, nilipata ono lake sio muda mrefu uliopita, nami nikauona, na nikawaona wapendwa wangu kule, wakiwa vijana tena. Upo. Upo. Ninajua upo! Naam, bwana! Sasa, labda mlilisoma kwenye gazeti la *Sauti* ya Wafanya Biashara Wakristo, na magazeti mengi na kadhalika yaliliandika. Enyi marafiki, hilo halikuwa ni ono. Nimeona maono, ninajua, ninapaswa kujua yana nini, kwa makumi elfu ambayo amenipa. Bali hili halikuwa ni ono. Nilikuwa kule, nimesimama moja kwa moja pale, nikiangalia nyuma. Nami ninajua upo. Upo, enyi marafiki, upo! Ninajua upo! Naam bwana! Hakika tu kama vile ninavyosimama hapa, basi nisaidie, kama nina akili yangu timamu na nimesimama hapa katika mimbara hii, upo! Mungu ametoa ahadi Yake, nayo ni ya kweli, ni jambo la kweli kabisa! Naam, bwana. Upo. Angalieni.

105 Sasa tunaona, watu hawa waliketi na wakala. Kisha wawili wao wakaamka wakashuka kwenda Sodoma. Mmoja alibaki na Ibrahimu. Hebu na tuangalie mazungumzo yao. Walikaza kuangalia Sodoma. Naye Ibrahimu alijua kulikuwa na kitu fulani kidogo kisicho cha kawaida kuhusu jambo hilo. Kwa hiyo akasema, hapo Yeye alipokuwa tayari kuondoka, Yeye alisema, "Mnafikiri ninapaswa kumficha Ibrahimu; kwa kuwa atakuwa baba wa mataifa, ninajua jinsi atakavyowalea watoto wake, na kadhalika; jambo nitakalofanya?" Akasema, "Dhambi za Sodoma zimekuwa mbaya sana mpaka tayari zimeingia masikioni Mwake." Alishuka kuja kuchunguza.

106 Sasa kumbukeni, kama nilivyosema hivi majuzi usiku, wawili wa wajumbe hao walishuka wakaingia Sodoma, nao

wakawahubiria hao Wasodoma; nao wakawapofusha usiku huo, kwa Neno. Lakini, kumbukeni, kulikuwako na Mmoja, wao, walikuwa na ishara yao, Mgeni miongoni mwao.

107 Mwangalie Lutu. Lutu akiketi langoni, na akasema, "Bwana zangu." Na akiishi jinsi hiyo! Wao wakasema, "Njoni nyumbani kwangu." Akasema, "Tutalala mtaani." Ni nyumba ya jinsi gani!

108 Lakini mara tu Ibrahimu; wao walisema, "Hili ndilo kusudi lililotuleta. Tutaketi hapa karibu nawe."

109 Hiyo ndiyo njia. Ishi hivi kwamba, kwamba kama Mungu angetaka kukutumia, Yeye anajua mahali hasa atakapokuja kukupata. Uko katika hali, unaishi maisha safi mbele za Mungu, maneno yako ni ya kweli, maisha yako ni ya haki. Hapo ndipo aina ya mahali Malaika wanapokuja. Mwangalie E—Elisabeti na Zekaria, unaona, mtu mwaminifu na mnyofu, akitembea katika Amri zote za Bwana. Hivyo ndivyo tunavyotaka kuishi, ili kwamba Mungu anapokuwa tayari kututumia, Yeye atasema, "Hawa ni watu Wangu. Ninaweza kufanya na kanisa hili yale ninayotaka kufanya. Wananiamini. Wanasimama kwenye Neno Langu." Unaona, hivyo ndivyo jinsi unavyotaka kufanya, kuishi maisha yapaswayo.

110 Sasa tunaona ya kwamba Malaika huyu, Yeye alisema, "Sitamficha Ibrahimu. Bali nitakurudia majira kama haya mwakani." Na, angalia, Yeye hakumwita *Abramu*, alimwita "Ibrahimu." Alijuaje ya kwamba jina hilo lilikuwa limebadilishwa? Yeye Ndiye aliyelibadilisha. Hakika. Angalia, kamwe hakumwita *Sarai*, mwajua, S-a-r-a-i. S-a-r-a, "Yu wapi Sara, mkeo?" Alijuaje alikuwa ameoa? Alijuaje alikuwa na mke, na jina lake lilikuwa ni Sara?

Ndipo Ibrahimu akasema, "Yumo hemani nyuma Yako." Ni mama halisi jinsi gani!

111 Siku hizi, wanawake ni wajeuri sana! Kila. . .Waume wao hata hawawezi kuzungumza. Wanajianika huko nje, sigara mkononi mwao, wamevaa kaptura, ni wao tu wanaozungumza. Ni jamii ya watu iliyopotoka jinsi gani, hana budi kuwa ndiye mpishi mkuu na mwosha chupa, chochote kile! Anapoondoka jikoni, anaondoka kwenye jukumu lake, kweli, kama mama.

112 Sasa tunaona, wanawake siku hizo walibaki nyuma na kuwa na adabu njema, walitenda kama mama wa heshima, kichwa chao ndicho kilichofanya maamuzi na kadhalika.

113 Nawe unajaribu kumwacha mtu fulani amwambie mkewe; mke atasema, "Nitakufanya uelewe sasa hivi!" [Ndugu Branham anapiga mbinja—Mh.] akipuliza moshi huo toka mdomoni mwake, akionekana hivyo, jinsi anavyoonekana na sura mbaya sana. Sijapata kuona kitu kama hicho! Nanyi mnaweza kuwazia huko nje, na kusimama pale ukimwangalia mtu huyo, uitambue roho hiyo pale, na vitu hivyo; na labda anaimba katika kwaya katika kanisa fulani. Loo, ni siku ya jinsi gani tunayoishi! Si

ajabu tuko kwenye siku hiyo! Na—natumaini mnaweza kushika kwenye mistari kile ninachomaanisha.

114 Angalia, hivyo ndivyo ilivyokuwa. Sara alikuwa hemani, alikaa kule ndani na akajiheshimu. Ibrahimu alikuwa akiwakaribisha Malaika hawa. Sasa, Yeye alisema, "Nitakuzuru."

115 Naye Sara alikuwa akisikiliza. Naye akacheka kifichifichi, akasema, "Mimi, mama kizee, nikiwa mkongwe hivi, na hapo bwana wangu ni mzee pia, na kusema ya kwamba tutapata furaha tena kama mume na mke?" Naye akacheka.

116 Naye Malaika, akiwa ameugeuza mgongo wake, akasema, "Kwa nini Sara amecheka?"

117 Kumbukeni, hiyo ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho ambayo Uzao wa. . .ama Ibrahimu mwenyewe, ambaye ni mfano wa Kanisa, ilikuwa ndiyo ishara ya mwisho aliyoipokea. Kutokana na ishara zingine zote alizopata, hiyo ilikuwa ndiyo ya mwisho kabla Sodoma haijafagiliwa mbali. Hiyo ni kweli? Ishara ya mwisho!

118 Wakati Israeli, ule uzao uliomfuata Ibrahimu. Na Wasamaria, ambao ulikuwa ni uzao uliotupwa uliotokana na mchanganyiko wa mbegu, wakimtarajia Yeye, hata hivyo; wao walisema, "Baba ye—yetu Yakobo alitupa kisima hiki," mwanamke yule alisema kule Sikari. Unaona. "Baba yetu Yakobo, yeye—yeye alimpa Yusufu kisima hiki, mwanawe, na—nasi tumekinywea, naye aliwanywesha ngamia wake. Nawe unasema ati Wewe una maji, kitu kama hicho?" Unaona? Na ishara ya mwisho ambayo uzao wa Israeli, wa kawaida, uliyopokea, ilikuwa ni ishara kama hiyo! Whiu! Hamwezi kuliona? Wazieni kwa dakika moja!

119 Ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu akiwa na lile agano, ishara ya mwisho kabla ya kukataliwa kwa kanisa vuguvugu, na maangamizi yake, ilikuwa ni ishara ya kuyatambua mawazo moyoni na niani, Mungu akidhihirishwa katika mwili wa kibinadamu.

120 Nayo ishara ya mwisho ambayo Israeli iliona kabla ya kukatiliwa mbali, ilikuwa ni jambo lile lile. Nao wakasema, "Ni Beelzebuli; mpiga ramli."

121 Hii ndiyo ile saa! Mungu, jalia hili lizame ndani! Sasa hii ndiyo ile saa, ambayo, ule Uzao wa kifalme wa Ibrahimu! Mnalipata? Mungu akidhihirishwa katika mwili wa kibinadamu, akiwapa ishara yao ya mwisho kabla ya kule kuangamizwa kwa walio vuguvugu na kuondoka kama ilivyofanyika huko nyuma. Ya mwisho! Fahari ya mwisho ya kurudi nyuma kwa Lutu! Hebu hilo lizame kwa dakika moja.

122 Ibrahimu, mmoja; uzao wa maumbile ya kawaida wa Ibrahimu, mbili; Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, tatu.

123 Angalieni, Ujumbe hauambatani na walio vuguvugu huko nje. Ni wapi ambako hata uliwaendea? Ulitumwa kwa wapentekoste, wateule, waliovutwa wakatoka.

124 Na kama vile Israeli ilivyofanya wakati huo, tisini-. . . Angalia ni wangapi, angalia ni Israeli wangapi walioupokea. Wakati ulipowadia wa wao kwenda kule juu, kulikuwa na mia moja na ishirini kutoka kwa karibu milioni nne.

125 Sasa angalieni ule Uzao wa kifalme. Unaona, hauna budi kuja mara hizo tatu, unaona, kila mahali unapopachukua. Watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Uzao wa kifalme wa Ibrahimu! Huyo hapo Ibrahimu; uzao wa kawaida; uzao wa kifalme. Kila kitu! Uzao wa kifalme ni kwa Kristo, kupitia . . . Tunakuja kwenye ahadi ya Ibrahimu ambayo Mungu alimpa kupitia kwa Kristo, ule Uzao wa kifalme. Na huu ndio Uzao wa kifalme, Kanisa hili la Bwana Yesu ambalo analirudisha katika siku za mwisho. Uzao wa kifalme! Angalia, yeye aliipokea ishara hiyo! Naye Uzao wa kifalme Mwenyewe alisema, wakati alipokuwa hapa, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Uzao wa kifalme, Uzao wa Ibrahimu, ulioitwa utoke; Lutu pia, wa ndugu yake, vuguvugu, huko chini Sodoma; halafu Wasodoma, ulimwengu. Leo hii, ulimwengu; ulimwengu wa kanisa; na Uzao wa kifalme. Barabara kabisa, wako mahali pao na kadhalika, kulingana na utaratibu kabisa. Naye Mungu, akiwa na ahadi Yake, ameshuka moja kwa moja, akidhihirisha jambo lile lile. Amina. Kama si kamilifu, sijui ukamilifu ni kitu gani. Ni Maandiko!

126 Mmekuwa na kunena kwa lugha, kucheza katika Roho. Mmekuwa na mihemuko hii yote mliyokuwa nayo, mmeona miujiza ya uponyaji, na—na viti vya magurudumu, na kadhalika. Tumeona hayo yote. Lakini hapa, hii hapa ishara ya mwisho ambayo imejitokeza sasa. Ibrahimu aliona kila namna ya mambo aliyofanyiwa na Mungu safarini, hakika, lakini hii hapa ishara ya mwisho inakuja, kabla tu ya kuja kwa yule mwana aliyeahidiwa. Na sasa Uzao wa kifalme unamtazamia Mwana aliyeahidiwa. Haleluya! Je! sisi, sisi tunamtazamia Mwana aliyeahidiwa? Mwana wa Mungu kurudi! Haleluya! Loo, hilo linanifanya kujisikia kama kupaza sauti. Angalieni! Ule Uzao wa kifalme unamtazamia Mwana aliyeahidiwa. Kama vile Ibrahimu alivyofanya katika miaka hiyo yote, akiangalia, akilishikilia hilo Neno, vivyo hivyo na Uzao wa kifalme. Nao huo Uzao ukimtarajia Mwana huyu ajaye, kuja kwa Bwana, kupitia zamu moja, zamu ya pili, zamu ya tatu, hadi kufikia kwenye zamu ya saba, nasi hapa tungali tunautarajia ule Uzao wa kifalme. Basi tunaona kitu gani kabla tu ya kule Kuja kwa Bwana? Ni kitu gani kinachotukia? Mungu anashuka miongoni mwetu, akiuonyesha Uzao wa kifalme kama alivyouonyesha uzao wa Ibrahimu; na Ibrahimu, na uzao wa Ibrahimu, na Huu

hapa pamoja na Uzao wa kifalme. Mungu akikaa miongoni mwetu katika umbo la Roho Mtakatifu, akifanya mambo yale yale aliyofanya huko nyuma, akifanya, akionyesha ni jambo lile lile.

Na kwenye utafiti wa kisayansi kwenye picha ile, ulimwengu unajua, ulimwengu wa kisayansi unajua hiyo ni kweli.

Kanisa linajua kwamba hiyo ni kweli, kote ulimwenguni.

127 Nami ninaamini ya kwamba kila Uzao uliochaguliwa tangu awali karibu umeingia, mlango uko karibu kufungwa, na hukumu inakaribia kupiga. Hiyo ni kweli. Mungu daima hatashindana na mwanadamu. Atafanya yote awezayo. Lakini saa inakaribia, enyi marafiki. Angalieni.

128 Nitawapa jambo fulani la kuwasaidia sasa. Kumbukeni, je! ni jambo gani lingine lililotukia sasa? Kabla hawajaweza kupokea uzao wa kifalme, ilibidi mwujiza fulani utukie kwa Ibrahimu na Sara pia, kimwili, kabla hapajaweza kuwapo na uzao wa kifalme. . . ama kabla uzao huo haujazaliwa. "Sasa, mwili wa Ibrahimu ulikuwa kana kwamba umekufa," Biblia inasema hivyo. Sivyo? "Na tumbo la uzazi la Sara lilikuwa limekufa," Biblia ilisema hivyo. Sasa ilibidi kutokee kitu fulani cha kimwili kabla huo uzao wa kifalme haujaninii . . . uzao haujatokea, yule mwana aliyeahidiwa. Kabla huyo mwana aliyeahidiwa kutokea, ilibidi jambo fulani la kimwili litukie mwilini mwao, kabla ya kuonekana kwa huyo mwana aliyeahidiwa. Angalia yale aliyofanya. Nitawapa kitu fulani kidogo.

129 Sasa, unaposoma Biblia, Hiyo ni Hadithi ya mapenzi ambayo Mungu aliliandikia Kanisa Lake. Ni Mungu. Mungu ni upendo. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nayo Biblia imeandikwa ili kwamba wasomi na wenye bongo hawawezi kuifahamu kamwe. Inakubidi kuwa unapendana na Mungu kusudi uielewe. Inakupasa kuwa na Mungu ndani yako. Yeye hujifasiri Mwenyewe kwako.

130 Sasa, ni kama vile tu nilivyo na mke. Loo, jinsi ninavyompenda! Ninampenda kwa moyo wangu wote. Nami nitakuwa katika nchi za ng'ambo mahali fulani naye ataninii . . . baada ya yeye kuwapeleka watoto kulala, ataniandikia barua, na kusema, "Mpenzi Billy, nimeketi hapa usiku wa leo, ninakuwazia. Ninaandika." Unaona, ninajua yale anayoandika kwenye hiyo karatasi. Bali ninamjua na ninampenda sana hata ninaijua tabia yake, ninajua yale anayomaanisha, kwa hiyo ninaweza kusoma katikati ya mistari. Unaona?

131 Pia Mungu analitaka Kanisa Lake lisome katikati ya mistari. Sio kusoma *chochote* kutoka Kwake sasa! Inakupasa kusoma katikati ya mistari kuona yale linachomaanisha. Sasa angalia na uone, angalia kama sivyo.

132 Sasa, kile Mungu alichowafanyia Ibrahimu na Sara, Yeye anawaonyesha, mfano wa Kanisa Lake. Yeye aliwafanyia, aliwageuza wakawa kijana mwanamume na mwanamke. Hakika, alifanya hivyo, akawarudishia ujana wao tena, kama tu vile atakavyomfanyia kila Uzao wa Ibrahimu. Haidhuru wewe ni mkongwe na umevunjika-vunjika jinsi gani, ipo siku inayokuja ambapo utakuwa kijana na mwenye sura nzuri tena, hiyo ni kweli, uzuri wa hali ya juu kabisa wa maisha.

133 Nilimwuliza daktari si muda mrefu uliopita, "Niambie, bwana. Kila ninapokula, ninafanya upya maisha yangu."

Akasema, "Naam, bwana, hiyo ni kweli."

134 Nikasema, "Sasa, Mungu alisema ya kwamba 'tulifanywa kutoka katika mavumbi ya nchi.'"

135 Akasema, "Hiyo ni kweli. Mboga na nyama na kadhalika unayokula ni mavumbi. Ambapo unapata potashi na kalisi na kadhalika katika vitamini zako, ndipo basi unazitoa moja kwa moja kutoka nchini. Nawe umeumbwa kwa mavumbi ya nchi."

Nikasema, "Mmh. Sasa, Mungu aliiumba hivyo kwanza."

136 Akasema, "Sijui lolote juu ya hilo, lakini" kasema "ninajua kwamba sasa unakula chakula nacho kinajenga mwili wako."

137 Nikasema, "Nakuuliza." Nikasema, "Halafu unaniswali juu ya kuzaliwa kibikira?"

Akasema,"Naam, bwana, nikakuswali."

138 Nikasema, "Ningetaka kukuuliza jambo fulani, daktari. Nielezee jambo hili."

139 Akasema, "Vema, chochote kisichoweza kuthibitishwa kisayansi si cha kweli."

140 Nikasema, "Nitachukua upande wa pili, ya kwamba chochote kinachothibitishwa kisayansi si cha kweli, hakina maana yoyote." Ndipo nikasema, "Vitu pekee vilivyo halisi maishani ni vitu visivyoweza kuthibitishwa kisayansi: upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, saburi, imani. Kithibitishe kisayansi kwangu? Hata hivyo ni kitu halisi! Mungu, Roho Mtakatifu, Malaika!" Amina! "Imani hufanya mambo hayo. Kila kitu unachoona kinatoka ardhini, kinatoka kwa mama ardhi, kinarudi vivyo hivyo." Nikasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani. Nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, nilikula chakula kile kile ninachokula sasa hivi. Nilikula maharagwe, viazi, na mkate, na nyama. Na kila wakati nilipokula, nikawa mkubwa na mwenye nguvu zaidi."

Akasema, "Hakika, ulikuwa ukiyafanya upya maisha yako."

141 Nikasema, "Ni kwa nini, baada ya mimi kupita umri wa kama miaka ishirini na miwili, mtu mwingine yeyote, haidhuru mtu unakula kiasi gani, unakuwa dhaifu na mzee zaidi? Wazia jambo hilo." Nikasema, "Nina jagi la maji

hapa, na nina glasi; nami nilianza kumwaga maji kutoka kwenye jagi hili kubwa mno na kuyamiminia kwenye glasi hii, nayo ikaanza kujaa mpaka ikafikia nusu; halafu bila ya chochote hapa chini kamwe, jinsi ninavyozidi kuyamiminia ndani, ndivyo yanavyozidi kupungua. Haidhuru ninakula kiasi gani, jinsi ninavyokula vizuri; ninakula vizuri zaidi sasa kuliko nilivyokuwa nikila, vizuri zaidi mara mia kadhaa."

142 Ninajua jinsi ilivyokuwa kutafuna nyama ya ngozi usiku kucha, na kula kiamshakinywa cha ugali wa mahindi pamoja na molasi ya mtama, na kula kitu kile kile kwa chakula cha mchana na usiku, pia. Ninajua ilivyokuwa kuishi maisha magumu, na sasa ninaweza kula vizuri zaidi. Namshukuru Bwana. Lakini haidhuru ninakula kiasi gani, ningali ninakuwa dhaifu na mkongwe zaidi. Na hatimaye nitakauka na kufa. Kwa nini? Kwa nini? Ni mapatano Mungu amefanya. Hiyo ni kweli. Naam, bwana.

143 Na hebu waangalie Ibrahimu na Sara, walirejea kwenye umri wa miaka ishirini na miwili ama ishirini na mitano.

144 Loo, mnasema, "Upuuzi, Ndugu Branham!" Vema, sasa ketini kimya kwa dakika moja, hebu na tusome katikati ya mistari mara moja.

145 Mara baada ya hao Malaika kuondoka, na Sodoma kuteketezwa, Ibrahimu na Sara walisafiri mwendo mrefu wakashuka moja kwa moja kwenda Gerari. Hiyo ni safari ndefu sana kwa mume na mke wakongwe. Hebu ipime kwenye ramani yako. Walishuka wakaenda Gerari. Na huyu hapa Sara sasa, bibi, mwenye umri wa miaka tisini, amevaa kijikofia cha kujikinga na jua, anatetemeka. Na Ibrahimu akiwa na ndevu zake ndefu zikining'inia chini. Biblia ilisema, "Wote wawili walikuwa ni wazee wenye umri mkubwa." Usijaribu kusema ya kwamba waliishi muda mrefu zaidi. Na Biblia ilisema, "Miili yao wote wawili ilikuwa imekufa, ni wazee sana." Nao hawa hapa wanashuka kwenda Gerari. Na kuna mfalme kijana kule chini jina lake Abimeleki, naye alikuwa akimtafuta mpenzi, na alipomwona Sara akampenda. Hiyo ni kweli? Bibi?

146 "Mbona, wewe umewazidi wote!" Ibrahimu akasema, "Wewe una sura nzuri ya kutamaniwa." Amina. "Nakuomba, mwambie wewe ni—ni dada yangu." Haleluya! Yeye alikuwa akionyesha hapo yale atakayoufanyia Uzao wote wa Ibrahimu. Sara alikuwa na sura nzuri. Ibrahimu alikuwa kijana. Ninaweza kumsikia Ibrahimu akisema, "Sara, mpenzi, wajua nini, mvi zinaondoka kwenye nywele zako."

147 "Ibrahimu, nundu inatoweka mgongoni mwako. Unanyoka." Walirudi wakawa kijana mwanamume na kijana mwanamke. Mungu, akionyesha! Loo, jamani!

148 Ndipo Abimeleki akampenda, kisha akaenda akamchukua, angalimwoa. Ninaweza kumwona akioga, kisha analala na

pajama zake, na kuinua juu vidole vyake vya miguu, baada ya kuomba dua zake, na kusema, "Kesho nitamwoa yule mrembo wa miaka mia moja"? Kichekesho! "Yule msichana mrembo wa Kiebrania! Loo, ndugu yake, yule jamaa mdogo! Na jinsi dada yake alivyo mrembo!"

149 Ndipo Mungu akamtokea katika ndoto, na kusema, "Wewe ni kama tu mtu aliyekufa."

Kasema, "Bwana, ni kwa nini hivyo?"

Akasema, "Huyo ni mke wa mtu."

150 Akasema, "Ulijua uaminifu wa moyo wangu, Bwana. Akasema, 'Huyo ni kaka yangu.' Kisha naye akasema, 'Ni dada yangu.'"

151 Akasema, "Ndiyo, ninajua uaminifu wa moyo wako, hiyo ndiyo sababu nikakuzuia usinitende dhambi." Lakini sikilizeni! "Bali wewe ni kama mfu, na taifa lako lote limekwisha. Mumewe ni nabii Wangu. Sijali wewe ni mtakatifu jinsi gani, unaomba kiasi gani, sitayasikia maombi yako. Bali mumewe ni nabii! Nenda, na ukamrudishe mkewe na umwache akuombee. Usipofanya hivyo, utakufa." Haleluya!

152 Ilikuwa ni kitu gani? Mungu akiwaweka tayari Ibrahimu na Sara kumpokea mwana aliyeahidiwa. Ikionyesha ya kwamba jambo linalofuata baada ya dhihirisho la Malaika huyu wa Mungu, Roho Mtakatifu akionyesha ishara Yake ya mwisho, jambo linalofuata, huu unaopatikana na mauti unachukua wa kutopatikana na mauti nasi tunanyakuliwa juu hewani kumlaki yule Mwana aliyeahidiwa, Uzao wa kifalme wa Ibrahimu. Utukufu kwa Mungu! Haleluya! "Kwa kuwa tutabadilishwa kwa dakika moja, kufumba na kufumbua jicho, nasi tutanyakuliwa pamoja kumlaki Yeye hewani. Na hivyo tutakuwa pamoja Naye milele, yule Mwana aliyeahidiwa." Haleluya!

153 Loo, sitaufikia . . . Nitaninii . . . Labda kesho usiku nitaufikia mlango wa 22, unaona.

154 Loo, ninalipenda, nanyi je? Nina furaha sana, mambo haya yote! Biblia imejaa tu hivi vipande vya thamani vya dhahabu. Nyosha tu mkono uviokote, uvipanguse mavumbi na uviangalie. Kila kimoja cha hivyo kinamwakilisha Yesu Kristo, kila mtu, kwa kuwa ndani Yake mlikaa utimilifu wa Mungu. Ndani Yake, kila kitu kinaelekeza kwake. Kila kitu kutoka katika Agano la Kale kilielekeza kwenye msalaba; na kipo katika Agano Jipya, kinaelekeza nyuma kwenye msalaba. Hiyo ni kweli. Yote yako pale. Lo!

Kibarikiwe kifungo kifungayo
Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
Ushirika wa watu wenye asili moja
Ni kama wa huko juu.

155 Jinsi ninavyompenda! Jinsi ninavyotaka kumwona! Jinsi ambavyo ninatamani na kuungojea mwili huu mzee uliopigwa-pigwa, uliochubuliwa ukavunjwa-vunjwa, ukararuliwa ubadilishwe moja ya asubuhi hizi! Parapanda italia na wafu katika Kristo watafufuka. Tutanyakuliwa pamoja nao, kumlaki Bwana hewani.

156 Jinsi ambavyo Rebeka alimnywesha ngamia huyo wakati wa jua kupunga. Elieza hakumpata asubuhi. Hakumpata wakati wa adhuhuri; alimpata kwenye nuru ya jioni. "Itakuwa Nuru wakati wa jioni!" Kweli! Hapo ndipo alipompata. Akaufunika uso wake. Hakuwa na kichwa; alikuwa akienda kwenye kichwa chake. Amina. Mwanamke, ni tabia yake, ya mwanamke, kujisalimisha kwa mwanamume. Na ni tabia ya kanisa kujisalimisha kwa Kristo, kujisalimisha kwa mapenzi Yake. Kujisalimisha tu! Hana mawazo yake mwenyewe; yeye hulichukua Neno Lake, si la mtu mwingine. Kama Hawa angalifanya jambo hilo, isingetulazimu kamwe kufa; bali yeye alisikiliza hoja. Bali Bibi-arusi halisi wa Kristo huuchukua Uongozi wa Kristo, lile Neno, naye anaamini tu Neno la Mungu. Huyo ndiye Bibi-arusi halisi, aliyerejeshwa. Haleluya! Wakati umekaribia, enyi marafiki, umechelewa kuliko unavyowazia. Tuko katika wakati wa jioni. Roho Mtakatifu yupo hapa usiku wa leo. Ninajua ni maskini, kundi dogo kabisa.

157 Ungewazia, "Loo, kama kitu kama hicho kingetukia, Mungu angekidhihirisha huko Roma, kwa maaskofu na kwa mapapa. Angemjia askofu wa Kimethodisti. Angeenda kwenye seminari ya Kibaptisti. Angeninii . . . " Naam, hivyo ndivyo unavyowazia. Bali kamwe hakulifanya hivyo.

158 Yeye huja kwa wenye mioyo minyenyekevu, wale wanaomtazamia. Naye yupo hapa usiku wa leo, Roho Mtakatifu, Mungu, Malaika yule yule; hapa mbele ya wanasayansi, akithibitisha, huyo hapo amepigwa picha. George J. Lacy, mkuu wa hati za alama za vidole wa FBI, yeye alisema, "Nuru hiyo iligusa lenzi." Akasema, "Bw. Branham, nimesema mara nyingi ya kwamba ilikuwa ni saikolojia, ya kwamba ulikuwa ukiyasoma mawazo ya watu hao. Lakini" kasema "jicho la kimitambo la kamera hii halitapiga picha saikolojia. Nuru hiyo iliigusa lenzi. Ilikuwapo!" Hiyo hapo. Moja ya hizo imetundikwa huko Washington, D.C., imepewa hakinakili, "Kiumbe pekee cha kimbinguni kilichopata kupigwa picha kisayansi na kuthibitishwa."

159 Kwa nini? Kama nikifa usiku wa leo, nisipoingia kwenye mimbara hii kesho usiku, maneno yangu ni Kweli. Kwa sababu, siyo maneno yangu, ni Yake. Kamwe sijasema "mimi mwenyewe." Sio mimi. Nisingeweza kufanya lolote. Mimi ni mwanadamu kama mlivyo ninyi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema. Lakini Mungu, katika siku hizi za mwisho, aliahidi mambo haya, nayo haya hapa! Ni Neno. Kama ingekuwa ni hadithi fulani za uongo, huenda ingekuwa ni tofauti. Lakini

ni Neno likithibitisha Neno kwa Neno, likiyakinisha, Biblia nzima. Imethibitishwa na wanasayansi! Imethibitishwa na Roho! Imethibitishwa na kanisa! Mungu miongoni mwetu! Haleluya. Ninafurahi sana kwa ajili ya jambo hilo. Ninyi hamna furaha, jana usiku, mlisimama na kuuchukua msimamo huo? Je! liliwafanya mjisikie wa tofauti? Sikuzote litawafanya hivyo, mnapolitetea Neno la Mungu. Mteteeni Kristo! Msilionee aibu.

Na tuombe.

160 Kuna mtu hapa usiku wa leo ungetaka kuinua mkono wako kwa dakika moja sasa, na kusema, "Ndugu Branham, nikumbuke katika maombi yako. Nitaninii, nina shauku sana kuwa mmoja wa hao Wazao wa Ibrahimu. Si—sitaki kukosa Mbingu. Omba, Ndugu Branham. Daima ndani ya moyo wangu nimejisikia kana kwamba kulikuwa na kitu fulani nimetaka nikipate. Kamwe sijaweza kukipata. Niombee, Ndugu Branham, ya kwamba Mungu atanipa kitu hicho"? Mungu akubariki. Iangalie tu mikono hiyo, kila mahali, ikiinuliwa.

161 Vipi huko kwenye roshani? Sasa, kumbukeni, Mungu ni mkubwa tu kwenye roshani kadiri alivyo mkubwa hapa chini.

162 Je! wewe kweli ni mwaminifu, unamaanisha jambo hilo? Inua mkono wako. Mungu akubariki. Ninaangalia tu kwa dakika moja. Endeleeni tu kuomba, endeleeni kuviinamisha vichwa vyenu.

163 Mwenye dhambi hapa ndani usiku huu ungetaka kuinua mkono wako, useme, "Nikumbuke, Bwana. Siuinui mkono wangu kwa ajili ya yule mhubiri; ninakwinulia Wewe mkono wangu. Kwa kweli ninaamini ya kwamba Wewe u hai leo, ya kwamba kamwe hukufa; ya kwamba wakati ulipokufa, ulifufuka tena, hasa. Na Wewe u hai milele, yeye yule jana, leo, na hata milele. Ninakwinulia Wewe mkono wangu, kwa kuwa ninaamini Wewe upo hapa"? Inua mkono wako, useme, "Nikumbuke, Bwana." Endeleeni tu kuomba. Mwaminini Mungu.

Aliyerudi nyuma, basi? Mungu akubariki. Yeye anaiona mikono yenu.

164 Baba yetu wa Mbinguni, unaiona mikono hiyo. Unajua kilicho nyuma ya hiyo. Ulisema, "Mpanzi alitoka akaenda kupanda Mbegu. Zingine zilianguka kando ya njia, hazikufaa kitu; zingine zikaanguka kwenye nchi yenye mawe; zingine kwenye miiba; zingine zikazaa mara mia moja." Huyo mpanzi aliwajibika tu kwa kupanda Mbegu. Jalia Roho Mtakatifu aikamate Mbegu hiyo sasa hivi. Bwana, sisi . . . Mimi—mimi naamini, Bwana, sisi . . .

165 Hakuna mtu ajuaye ni lini utakuja. Hatujui jambo hilo. Ulisema, "Hata Malaika hawatajua; ni Baba tu." Yesu alidai kwamba Yeye hakujua. "Ni Baba tu peke Yake."

166 Sasa, Baba, ninaomba ya kwamba kama kuna wale humu ndani walioinua mikono yao, ninaamini walimaanisha jambo hilo. Kuna Kitu fulani nyuma yao, ya kwamba, Roho, aliyewaambia wainue mikono yao, nao wakafanya hivyo. Wao ni waaminifu. Labda huu ndio wakati wa kwanza ambapo Wewe ulipata kunena nao, na huenda ukawa ndio wakati wa mwisho. Labda ulizungumza nyakati zingine, wala hutanena tena. Sijui. Lakini, Baba wa Mbinguni, ninaomba ya kwamba utampa wokovu kila mtu anayeamini.

167 Jalia Jina Lako takatifu liheshimiwe mbele za watu. Pendo Lako na limiminwe katika kila moyo na Roho Mtakatifu. Wabariki hawa ndugu wahudumu, Bwana. Watu hawa wa thamani hapa ambao, katikati ya mapambano, walinialika, haidhuru. Wabariki watu wanaohudhuria.

168 Simaanishi kuwa na kiburi, simaanishi kuwa wa tofauti, Bwana; kuwa mkweli tu. Na hilo ndilo jambo pekee utakalotambua, ni kweli iliyo ndani ya mtu, kwa maana Wewe ni Kweli. Sikia sasa, Baba, ninaomba. Wajalie usiku wa leo ya kwamba wengi wao hapa, ambao labda hawakuinua mikono yao, wataokolewa, haidhuru. Tujalie, katika Jina la Yesu. Amina.

169 Sasa tukiwa tumeketi kwa uchaji kwa dakika moja. Ninaamini tumechelewa kidogo kuwa na mstari wa maombi, lakini tutaufanya. Kila mtu, wakati ninyi. . .ninyi, kama una kadi, wewe ishikilie kadi yako. Kama huna kadi, chukua moja. Tunaninii. . .Kama itatubidi kukaa hapa siku tano za ziada, tutamwombea kila mmoja wao. Hiyo ni kweli.

170 Ninajaribu tu kuwaletea watu Ujumbe. Ninajaribu kuwafanya mwone ninii muhimu. . .Kama ukiponywa; labda, kama ukiishi muda mrefu vya kutosha, utakuwa mgonjwa tena wakati mmoja. Lakini kama ukiokolewa, una Uzima wa Milele. Unaona? Unaweza ukaponywa, na uende zako na uupoteze wokovu wako. . .ungeweza kuupoteza uhai wako, hasa; lakini wakati umeokoka, una Uzima wa Milele basi, kamwe hutakuwa mgonjwa.

171 Sijui kama mlielewa usiku wa leo kile nilichokuwa nikinena habari zake, ya kwamba Mungu aliwatokea Ibrahimu na Sara pale, na akawapa ishara ya mwisho, yule Malaika, hilo ni kabla ya yale maangamizi kutokea na yule mwana wa ahadi kutolewa. Kwa Kanisa, hiyo, ishara hiyo, ilikuwa ni kule kuja kwa Mwana. Kwa ulimwengu, ilikuwa ni maangamizi. Sasa, kile alichomfanyia Ibrahimu na hao wengine kilikuwa ni mifano.

172 Yesu alikuja duniani, yule Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, na akafanya ishara hiyo hiyo. Ni wangapi wanaojua kwamba ndivyo ilivyo, waseme, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.] Hakika. Nao wakaikataa. Hiyo ni kweli?

173 Sasa, Yeye kamwe hakufanya jambo hilo kwa Mataifa, maana Uzao wa kifalme haukuwa umetoka, Kanisa halikuwa

limezaliwa bado. Lakini wakati Kanisa lilipozaliwa, na sasa limekuwa na miaka elfu mbili, kwenye ninii tu . . . Kumbukeni, huko kulikuwa ni mwisho wa kungojea kwa Ibrahimu. Huo ulikuwa ni mwisho wa kumngojea Masihi kwa ule uzao wa kawaida, maana Masihi alikuwa pale.

174 Huku ni kumalizika kwa kungojea kwa Uzao wa kifalme. Yeye yupo hapa, kule kuonekana kwa Kristo. Je! ulipata kujaribu kugawanya . . . Kuna mahali katika Biblia, unajua, sina wakati wa kupaendea, panaposema, "kuonekana kwa Kristo," na halafu "Kuja kwa Kristo." Hayo ni mambo mawili tofauti, kabisa, kule "kuonekana" na kule "Kuja." Yeye anaonekana sasa, akitenda kazi nasi katika umbo la Roho Mtakatifu, akilifanya tu kamilifu, hilo Kanisa. Halina budi kukamilishwa.

175 Kama vile ukiwa na noti ya dola mfukoni mwako, uitoe na kuiangalia. Upande mmoja ni ule muhuri wa Marekani; upande huo mwingine ni muhuri wa Kimisri, ile piramidi ikiwa na jiwe la kifuniko huko juu yake kabisa, kama jicho linaloangalia. Na ni kwa nini dola ya Marekani iandike pale chini, "Ule muhuri mkuu"? Inaonekana kana kwamba muhuri wa Marekani ungekuwa ndio ule muhuri mkuu hapa. Lakini Serikali ya Marekani wanautambua watake wasitake, ule muhuri mkuu.

176 Iangalie hiyo piramidi wakati ikipata umbo ikipanda juu, lile Kanisa. Kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kisha hiyo haina budi kuchongwa kufikia mahali ambapo . . . Lile Jiwe la Kifuniko kamwe halikuja kwenye hilo piramidi, lilikataliwa, kama tu vile lile Jiwe la Pembeni. Sasa, lakini wakati hilo Jiwe la Kifuniko litakapokuja . . . Nimekuwa kwenye piramidi; limeshikamana kikamilifu kabisa, usingeweza kuingiza wembe kati yake, mahali ilipo mota. Na wakati Kanisa litakapokuja, hapo ni . . . Wakati Kristo atakapokuja kulipokea Kanisa Lake, hilo Kanisa litakuwa na huduma inayofanana kabisa na hiyo, na kwa neema hiyo litakifufua kitu hicho chote, kisha liondoke. Kule kuja kwa lile Jiwe la Kifuniko, likipaza sauti, "Neema, kwa Bwana!"

177 Nina jambo fulani moyoni mwangu. Haleluya! Mungu wetu angali ni Mungu. Yeye huwafunulia watumishi Wake siri Zake. Nilinena juu ya Malaika aliyeelekeza mgongo Wake kwenye hema, na mgongo wake ulikuwa umeelekea kwenye hema, na akasema yale Sara aliyokuwa akiwazia akiwa humo ndani. Ninabashiri ya kwamba Malaika huyo yupo hapa sasa, Roho Mtakatifu, Nguzo ile ile ya Moto, yeye Yule aliyekuwa ndani ya Kristo. Nguzo ya Moto iliwaongoza wana wa Israeli. Nguzo ya Moto ilifanyika mwili ikakaa kwetu. Yeye alisema, "Nilitoka kwa Mungu, naenda kwa Mungu."

178 Baada ya kifo Chake, kuzikwa, kufufuka, kupaa, Yeye alikutana na Sauli akienda zake Dameski. Ndipo Nuru ikampiga ikamwangusha chini. Naye akasema, "Bwana, Bwana!"

179 Akasema, “Sauli, Sauli,” kwanza. “Ni nani . . . Kwa nini unaniudhi?”

Kasema, “U Nani Wewe, Bwana?”

Akasema, “Mimi ni Yesu.” Amerudi!

180 Hapa Huyu hapa usiku wa leo, amethibitishwa na Kanisa Lake, kisayansi na yote! Loo, enyi marafiki, kwa nini sisi ni wazito wa akili hivi? Kwa nini tunaketi tumedhoofika sana? Hebu—hebu Mungu aliyenena hilo Neno, hebu Mungu aliyeninii . . . Kama vile Elisha alivyosema, aliyerudi akiwa na sehemu maradufu ya Eliya, alipolikunja lile vazi, na kusema, “Yuko wapi Mungu wa Eliya?” Hebu Mungu aliyeliandika Neno, alithibitishe Neno! Kama Hili ni Neno Lake, hebu na alitetee! Aliahidi kufanya jambo hilo. Yeye atalifanya kama tutaamini.

181 Sasa hebu niwajulishe jambo hili dhahiri. Mimi siye Mtu huyo. Mimi ni mtumishi wa Mtu huyo. Nanyi, pia, kama ninyi ni Uzao wa Ibrahimu.

182 Lakini, mimi nikilihubiri Neno Lake, na nikisimama katika siku ambayo kila dhehebu limenikataa, mashirika yananifukuza kutoka mahali pamoja hadi pengine. Na ndugu tu wa thamani walio kwenye mashirika hayo, ambao wanaiona Nuru, wataishikilia haidhuru makao makuu yanasema nini. Mungu awabariki watu kama hao. Mungu awabariki wanawake na wanaume waliosimama jana usiku. Niwafanyie nini? Niombeni jambo fulani. Niombeni la kufanya, nitawafanyia chochote niwezacho. Ninyi ni watu wa Mungu. Mwanamume ama mwanamke yeyote atakayechukua msimamo kama huo, katikati ya mashambulizi, ninakuheshimu.

183 Sasa kama Malaika huyo . . . Katika Neno la Yesu Kristo imetabiriwa, ya kwamba kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Adamu, ya kwamba jambo lile lile lililotukia huko Sodoma lingetukia katika Kanisa, hebu na ajitokeze jukwaani.

184 Nitageuza mgongo wangu. Wewe inamisha kichwa chako na uombe. Kamwe nisingesema jambo hili kama sikujisikia kuongozwa kulifanya. Ningekuwa mpumbavu kwa kutoa tamshi kama hilo. Lakini, nikimwamini Kristo Mwana wa Mungu, nikiamini ya kwamba Yeye ni Neno! Nalo Neno limefanywa halisi katika miili yetu, tunapolichukua Neno, kwa maana ni ahadi Yake, “Nitakuwa ndani yenu hata ukamilifu wa dahari, na kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya.”

185 Nimegeuza mgongo wangu uelekee kwa wasikilizaji, Baba wa Mbinguni, ambao nimewahubiria, juu ya Ujumbe huu. Ninakuomba Wewe, Mungu, jalia ijulikane usiku wa leo ya kwamba Wewe ungali Yesu Kristo Mwana wa Mungu, na ungali u Yehova Mungu. Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na ilikuwa ni Wewe pale ukiongea na Ibrahimu siku ile hemani. Ilikuwa ni Wewe ambaye uliweza kutambua kile mwanamke yule alichokuwa akiwazia hemani, na ukamwambia.

Na wakati uo huo, yeye akikana, Wewe ungaliutwaa uhai wake, bali alikuwa ni sehemu ya Ibrahimu, bibi-arusi wake. Bwana, Wewe ungeyatwaa maisha yetu, kwa ajili ya kutokuamini kwetu, bali sisi ni sehemu ya Kristo. Usingalimchukua, usingaliweza kumwangamiza Sara, bila kumdhuru Ibrahimu. Wala huwezi kuliangamiza Kanisa bila—bila kumdhuru Kristo. Nisaidie, Bwana. Sina elimu. Mimi ni ninii tu. . . Bwana, sina kitu, bali ni kukuamini Wewe tu. Nami ninaamini. Isaidie, Bwana.

186 [Dada fulani ananena kwa lugha nyingine. Dada mwingine anatoa tafsiri—Mh.] Amina. Mungu aliye hai na ashukuriwe. Sasa, Yeye yupo. Iweni na kicho, heshima.

187 Unaweza kuinua kichwa chako kama ukitaka. Sasa si kwamba tu. . . Unaona, Biblia inasema kwamba kunena kwa lugha ni kujijenga tu mwenyewe, isipokuwa pawe na ufasiri. Na kama huo ufasiri, huo ni unabii kwa Kanisa. Na jinsi nilivyouelewa huo ufasiri basi, ulikuwa ni "Mwaminini Bwana, ya kwamba Yeye Ndiye amelituma hili Neno." Na halafu sikuja kwa jina langu mwenyewe, nimekuja katika Jina Lake. Na kazi Zake atazifanya kupitia kwangu basi, kwa kulihubiri Neno Lake na kulithibitisha Neno Lake. Hakika. Ninaamini hilo. Je! mnaamini jinsi iyo hiyo? [Kusanyiko linasema, "Amina!"—Mh.] Ni wangapi wanaamini jambo hilo sasa, kabla Yeye. . .? Mungu awabariki. Sasa, hiyo ndiyo njia ya kuninii, hiyo ndiyo njia. Dumisheni huo usawa wa ufanani nanyi mtaona jambo fulani likitukia.

188 Nitageuza mgongo wangu uelekee kwa wasikilizaji, kwa sababu huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu akishuhudia tu jambo hilo. Unaona? Iweni imara kwa kile mfanyacho. Sasa wewe amini huko nje katika wasikilizaji, mtu fulani. Hakuna mtu ninayeweza kumwona. . . Ni wangapi huko nje walio wagonjwa na wanateseka, ama wana mtu ambaye anateseka, ama kitu fulani ambacho unaombea, nawe unajua sijui lolote juu yake, inua tu mkono wako. Vema, nadhani ni karibu kila mahali. Vema, hebu na tuamini tu sasa. Kamwe, kamwe mtu yeyote asiondoke, nipeni tu. . . Ni—ni saa nne kasoro dakika kumi na mbili. Nipeni dakika kumi na mbili, sawa? Mtu yeyote asisogee. Mtu yeyote asiondoke, hata kidogo. Ketini tu kimya kabisa sasa. Wakati mmoja tu, ufungue moyo wako.

189 [Ndugu mmoja ananena kwa lugha nyingine. Ndugu mwingine anatoa tafsiri—Mh.] Amina. Asante, Bwana, asante. Kwa uchaji tunaliheshimu jambo hilo kwa moyo wetu wote. Hiyo ni karama Kanisani. Iweni tu katika maombi, kwa uchaji.

190 Kumbukeni, walikuwa wakienda vitani wakati mmoja, hawakujua jinsi ya kukabiliana na vita hivi vikubwa. Daudi alikuwa amesimama pale, naye akagawana nao kipande cha nyama na balasi ya divai. Lakini Roho alishuka juu ya mtu

mmoja, naye akatabiri na kuwaambia mahali watakapokutana na adui, na ikawa hivyo.

191 Tunakabiliana na vita vikuu, ndugu. Nasi tunasimama katika vita vikuu sasa hivi. Roho ameshuka na, juu ya mtu fulani, naye amewaambia jambo la kufanya, "kuamini." Anajaribu kuyaondoa mawazo yenu kwamba ni mimi. Unaona? Baadhi yenu hapana budi mnawazia ya kwamba ni Ndugu Branham akijaribu kufanya jambo fulani. Sio mimi; ni Yeye. Ninaninii tu. . .Karama ni kujisalimisha tu, kama vile kujiingiza kwenye gia fulani. Ni kama tu maikrofoni hii, ukiifungua, kitu fulani hakina budi kuzungumza kuipitia. Ni kama gia tu ndogo ninayofungua, kitu kidogo. Roho Mtakatifu! Siifungulii; Yeye huifungulia. Ndipo Yeye ananena; sio mimi. Sasa iweni na kicho na mwamini, kila mmoja wenu, na mwombe tu.

192 Sasa, kila mtu anajua ya kwamba Biblia ilisema ya kwamba "Yesu Kristo sasa hivi ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo ya udhaifu wetu." Kama hiyo ni kweli, kusanyiko na liseme, "Amina." [Kusanyiko linasema "Amina!"—Mh.] Je! Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule? Semeni, "Amina." ["Amina!"] Kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, Yeye angetenda vile vile. Hiyo ni kweli? ["Amina."] Amina. Sasa mngefanya nini?

193 Sasa, kunigusa mimi, isingeleta tofauti yoyote; mimi ni mwanadamu. Bali kumgusa Yeye, basi Yeye ni Roho Mtakatifu aliye *humu* ndani, ndipo anajibu na kuitumia midomo ya binadamu. Kwa sababu, Yeye ndiye Mzabibu, sisi ni matawi; Yeye hazai tunda; Yeye hulitia tu tawi nguvu.

194 Hiyo ni kusema, nigeuze tu mgongo wangu, kusudi mpate kuona kwamba mambo ambayo nimesema.

195 Sasa, wahudumu hawa hapa jukwaani, wanaomba. Mnaweza kuniangalia mkitaka. Hilo ni sawa. Kuona tu, mpate kujua ya kwamba wao wananinii tu. . .Maana, wewe ni mchungaji, wewe ndiwe unayewachunga kondoo hawa. Kwa hiyo, kusudi tu mpate kujua. Nami ninawataka mniombee, enyi ndugu. Maana, mnaona ninalomaanisha? Ninamwakilisha Kristo yeye yule mnayemtumikia. Nami ni ndugu yenu, raia mwenzenu wa Ufalme, pamoja nanyi ndugu. Nami nipo tu hapa. . .

196 Mnaona, sasa, sasa hivi Neno ambalo nimehubiri, mnaona, liko hatarini. Sasa hivi, kushindwa, huko ndiko Shetani angetaka kuona. Hilo tu ndilo analotafuta. Lakini Mungu si mshindwa. Iweni tu na kicho.

197 Sasa huku nimeugeuza mgongo wangu, ninataka mtu fulani. . .Hebu niugeuze, nimegeuka kabisa. Hebu niigeukie sehemu *hii*, kwanza, kisha nitakuja kwenye sehemu *hiyo* nyingine. Sasa mtu fulani huku nyuma; wapo wengi mno, inaonekana, wanaomba. Hapa nyuma hivi, mtu fulani na aombe

sasa, ambaye anataka kumwamini Mungu. Amini tu kwa moyo wako wote, nyuma hapa mahali fulani.

198 Sasa, Baba wa Mbinguni, ni—ninakuthamini Wewe katika jumbe Zako zote, kila kitu ambacho umefanya. Sasa nisaidie, Bwana. Mimi ni—mimi ni . . . kwa imani, ninakuamini Wewe, Neno Lako. Ninaamini ilikuwa ni Roho Wako aliyeniita mimi kufanya jambo hili. Sasa na ijulikane ya kwamba nimesema Kweli. Nimeshuhudia habari Zako, sasa shuhudia, Bwana, ya kwamba nimesema Kweli. Ninaomba katika Jina la Yesu. Amina.

[Dada fulani ananena kwa lugha nyingine—Mh.]

199 Baba Mungu, tunangojea fasiri ya hiyo. Ulisema, katika Biblia, kungekuwako na "zamu za watatu," na hiyo ni ya tatu. Sasa sisi—sisi tunaomba ya kwamba—ya kwamba Wewe utamjulisha mtu fulani aliye na karama za ufasiri. Ninakuachia Wewe, katika Jina la Kristo.

[Ndugu fulani anatoa unabii—Mh.] Asante, Bwana.

200 Sasa, huo ulikuwa ni unabii, sio ufasiri. Unaona, alisema zaidi ya yale mwanamke huyu alivyosema. Kuna fasiri inayokuja. Unaona, mtu huyo alikuwa ni nabii.

201 [Ndugu fulani anatoa fasiri—Mh.] Amina. Asante, Bwana.

Moja kwa moja nyuma yangu . . .

202 [Dada fulani katika kusanyiko anaanza kuomba—Mh.] Mungu, mjalie mwanamke huyo baraka, anazolilia. Kuwa tu . . .

203 Sasa uwe na kicho sana sasa, na uamini kwa moyo wako wote. Sasa, kwa Roho Mtakatifu, ninajaribu kulileta Neno ambalo nimehubiri, ambalo Yeye ameshuhudia ya kwamba litatimia. Sasa amini kwa moyo wako wote.

204 Yupo mtu fulani amesimama mbele yangu, ambaye ameketi nyuma yangu. Na ni mwanamke. Naye ana shida ya moyo. Pia ana mizio inayomsumbua. Yuko tu nyuma yangu. Kama mwanamke huyo hajasimama bado . . . Wasikilizaji wanaangalia; nimefunga macho yangu. Yeye anahusika pia juu ya mpendwa, huyo ni, mume wake anayeketi karibu tu na yeye; amepooza, ana mkongojo. Jina la mwanamke huyo ni Bibi Brumley. Amini kwa moyo wako wote. Simama na ukubali ulichoombea, nawe utapata ulichoomba. Simama kwa miguu yako. Je! amesimama? [Kusanyiko linasema, "Ndiyo."—Mh.]

205 Mungu akubariki. Simjui mwanamke huyo, sijapata kumwona maishani mwangu. Hatufahamiani? Kuna . . . [Mwanamke huyo anasema, "Ndiyo."—Mh.] Sasa waulizeni, nendeni mkawaulize kama hiyo ni kweli. Sasa kama huyo si Mungu yeye yule aliyekuwa kule chini kabla tu Sodoma, sijui ni kitu gani.

206 Mtu mwingine katika sehemu hii aamini sasa kwa moyo wako wote. Bwana Yesu. Yupo mwanamke anayeketi moja kwa

moja nyuma yangu. Ana haja kubwa sana. Anaomba Mungu ampe kitu fulani. Ni mtoto mchanga, anaombea. Yupo moja kwa moja nyuma yangu. Bibi Holm, simama na umwamini Bwana Mungu. Na endapo utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kumpata mtoto huyo mchanga unayemwombea.

207 Mwanamke anaingia, naye ni kiwete. Ameketi kwenye kiti cha magurudumu. Yuko nyuma yangu. Yeye hatoki sehemu hii ya nchi. Anatokea—anatokea Sacramento, Sacramento ya kaskazini. Amekuwa ni mgonjwa sana. Madaktari hawawezi kumsaidia. Ameishakuwa hospitalini. Amekuwa na upasuaji mara nyingi. Ana shida ya figo, shida ya mifupa yake. Ana wasiwasi tu, hata ana magonjwa mengi tu. Hawezi kabisa. Bibi Beeler, pale, inua mkono wako na uamini ya kwamba Bwana Yesu . . . na ufanywe . . . Mungu akubariki.

208 Je! mnaamini? Mungu yungali hai na anatawala. Kama unaamini hilo kwa moyo wako wote!

209 Huyu hapa maskini mwanamke mmoja, ninamwangalia ameketi hapa. Ana shida ya utumbo mpana. Jina lake, simjui. Lakini unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe u nani, mama? Bibi Berglund. Amini kwa moyo wako wote, nawe unaweza kufanywa mzima. Amini.

210 Huyu hapa mama anayeketi papa hapa, akimwombea rafiki ambaye ndiyo kwanza apate ajali ya barabarani. Ukiamini kwa moyo wako wote, unaweza kupata kile ulichoombea.

211 Kuna mama anayeketi pale akiwa anaumwa na kichwa. Unaamini kwa moyo wako wote? Unaweza kuwa mzima. Usitilie shaka. Amini tu. Kama Yeye si Mungu yeye yule, sijui Yeye ni nani. Yeye yupo hapa ku—kuninii, kama utalikubali na kuliamini.

212 [Dada mmoja ananena kwa lugha. Ndugu mmoja anatafsiri—Mh.] Amina. Bwana asifiwe.

213 Hivi hamwezi kutambua ya kwamba mpo Uweponi mwa Mungu? Fanyeni hivyo. Sasa nafikiri kile tunachopaswa kufanya sasa hivi, baada ya Roho kuwa akinena, "Njoni kwangu, niamininini Mimi, watu Wangu," nafikiri inatupasa kusimama kwa ajili ya wito wa madhabahuni sasa hivi, na kuwaacha wale wasiomjua Kristo waje hapa madhabahuni na kumkubali Yeye kama mwokozi Wako. Kama hujampokea Roho Mtakatifu, wewe njoo, pia, umpokee Roho Mtakatifu, kwa kuwa ni hilo tu litatukia. Hivi hamwezi kuja wakati tunapopata sauti; mtu fulani ataongoza uimbaji. Roho Mtakatifu amekuwa akizungumza. Mungu akubariki, dada. Hiyo ni kweli. Mtu mwingine na ajitokeze pamoja na mama huyu hapa. Njoo moja kwa moja huku endapo una hiyo . . . Mungu akubariki, dada. Kwenye Uwepo, ambapo Biblia, Neno, kuthibitishwa, karama, kila kitu kinafanya kazi, si ni jambo zuri sana sasa hivi? Njoni moja kwa moja madhabahuni. Shukeni mje kutoka

roshani. Ninyi msio na Mungu, msiojazwa na Roho, njoni sasa tunapoimba.

Yesu anapita huku,
Huku, leo,
Yesu anapita huku,
Anapita huku leo.

Yesu anapita huku,

Hivi huwezi kuja sasa wakati anapopita, Roho Wake akitenda kazi, akisema, "Njoo"?

. . . leo,
Yesu anapita huku,
Anapita huku leo.

214 Hivi wewe hutakuja wakati Yeye anapopita? Angalia kile anachofanya miongoni mwenu, akionyesha ya kwamba ni yeye yule. Ondokeni moja kwa moja, kila mtu asiyemjua, asiyezaliwa mara ya pili. Hivi hutakuja kumtafuta? Kumbuka, Roho Mtakatifu yuyo huyo anakujua wewe.

. . . huku leo.

Yesu anapita huku,
Huku, leo,
Loo, Yesu anapita huku,
Anapita huku leo.

215 Sasa hebu kila nafsi ije sasa isiyomjua Mungu, mtu usiye na hakika mahali unaposimama. Njoo huku. Msi—msiwe . . . Usiwe na dhana ya kiakili juu yake, ndugu, dada. Usifanye hivyo. Huenda ulifanya namna yoyote ya mhemuko. Huenda umekuwa na damu mikononi mwako, usoni mwako, huenda ulishikwa na mitetemeko, na kadhalika. Sina kitu dhidi ya jambo hilo, sasa, hayo ni sawa. Huenda umenena kwa lugha, huenda umecheza katika Roho, na uwe bado umepotea. Hiyo ni kweli. Inabidi iwe ni maisha yaliyozaliwa ndani yako, ambayo hulichukua Neno hili na kulifanya hai tena. Unaona, Kristo ni Neno. Na endapo huna imani bado ya kuingia katika hilo Neno na kuliamini, hivi si uje sasa.

216 Kama Kanisa la Mungu, wakati Nuru za jioni zikianza kuangazia huku chini, nao m—mti unaiva; Mungu alisema ataurudisha mti huo, mti ule ule wa kipentekoste, Imani ya namna ile ile, kila kitu kile kile walichokuwa nacho, mti huo utarudishwa tena; bila dhehebu, bila chochote, utakuja katika nguvu rahisi za Roho Mtakatifu, akiifundisha Biblia jinsi hasa alivyofanya. Tumeahidiwa mmoja katika siku za mwisho, mnajua, aje na kuirudisha ile Imani. Kwa hiyo ninaamini Yupo hapa usiku wa leo, katika umbo la Roho Mtakatifu. Njoni sasa, tunapoimba tena, kwa hiyo tutakuwa na uhakika tumefaulu.

217 Sasa kumbukeni, kama roho hizi . . . Ninyi Wapentekoste hakika mnaamini karama zenu za lugha na fasiri! Kama

hamwezi kuamini yale aliyofanya *hapa*, basi aminini lugha zenu na fasiri zake, za kuwaita madhabahuni. Hebu kila mtu na aje. Mkiona *lile* likitenda kazi, *hili* likifanya kazi, Mungu akifanya kazi, mbona, ni Mungu! Vipi mengine, hili hapa Neno hapa likilithibitisha, likisema ya kwamba ni Kweli. Njoni. Wakati mmoja zaidi sasa, nanyi njoni sasa.

Yesu anapita huku,
Leo, leo,
Yesu anapita huku,
Anapita huku leo.

218 Sasa hebu wale wanaomwamini Mungu, wahudumu watakatifu wa kweli na—na watumishi wa Kristo, waje, wakitoka, tunapoimba tena sasa. Sogeeni karibu na madhabahu, karibu na hawa hapa. Na hebu tuombe nao, pamoja. Njoni. Hivi hamtakuja hapa? Siwezi kuwafikia, kila mmoja, kwa mikono yangu. Ninawatakeni mje. Baadhi yenu ndugu wahudumu shukeni mwende miongoni mwao kule chini sasa, mpate kuwagusa na kuwawekea mikono. Vema. Ninyi mnaomjua Mungu, njoni, mkisogea huku juu, baadhi yenu ninyi wanawake na wanawake hawa, ninyi wanaume na wanaume hawa. Sogeeni huku juu sasa. Hili ni—ni agizo la Mungu. Sogeeni huku juu sasa, ninyi watu. Huo, huo ndio, huo ndio wakati. Baadhi yenu akina mama wacha Mungu na baadhi yenu ndugu wacha Mungu, sogeeni hapa sasa ili mweze kuweka mikono yenu juu yao, katika thibitisho, mkiweka mikono yenu juu yao wapate kumpokea Roho Mtakatifu. Vema. Sasa, haya basi. Haya basi.

219 Sasa, kwa nini mmekuja? Ni kwa sababu kwamba mnaamini. Mmeshawishika ya kwamba Mungu yuko miongoni mwetu. Yupo hapa usiku wa leo. Yupo hapa akifanya kazi katika ishara kuu na maajabu.

220 Sogeeni karibu kabisa, kila mtu. Njoni moja kwa moja ili watu waweze kupata nafasi zaidi. Sogeeni karibu kabisa. Wapo wengine zaidi wanaoshuka kuja kwenye marefu ya kanisa, mnaona. Sogeeni tu karibu.

221 Ni wangapi katika wasikilizaji wanahusika kuhusu watu hawa wanaosimama hapa sasa, juu ya wokovu wa nafsi zao, inua mkono wako. Vema. Hebu sote pamoja sasa, tuinue mikono yetu kwa Mungu, na tuombe dua.

222 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuletea Wewe usiku wa leo wasikilizaji hawa, pamoja na Roho Mtakatifu miongoni mwetu, aliyepo sasa, akilifanya Neno Lake liishi upya tena. Jaza kila moyo, Bwana. Njoo katika nguvu za Roho. Tujalie, Bwana. Tupilia mbali kila hofu, kila pepo mchafu. Ingia kwa nguvu za Mungu, na uchukue mamlaka juu ya nafsi hizi. Katika Jina la Yesu Kristo, ninawakabidhi Kwako kwa utukufu Wako.

YEHOVA-YIRE 2 SWA62-0706
(Jehovah-Jireh 2)
MFULULIZO WA YEHOVA-YIRE

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kingereza mnamo Ijumaa jioni, tarehe 6 Julai, 1962, katika Ukumbi wa Manispaa huko Grass Valley, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2015 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org